Jumatatu Januari 18, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580466

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US

**Nyama** ya 'kitimoto' yapigwa marufuku

UKURASA 5



**Polisi** atakayeshindwa kudhibiti wahamiaji haramu kutumbuliwa

UKURASA 5



**Pogba kutua Juventus Julai**

UKURASA 20

RIPOTI MAALUM

# Madereva wa mabasi, wenye hoteli kitanzini

• **Ni** kashfa abiria kuuziwa chakula bei ghali... *Endelea Ukurasa 3*



Rais Dk. John Magufuli, akiwasalimia vijana wadogo wa Kikatoliki baada ya Ibada ya Jumapili ya Pili iliyofanyika katika Kanisa Katoliki la Bikira Maria Parokia ya Chato mkoani Geita. **PICHA: IKULU**

## Mbaroni tuhuma kuua babu kikatili

UKURASA 2

## JPM aagiza kuzalishwa chakula kusaidia waathirika wa Covid-19

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** **MATOLA AMTABIRIA MAKUBWA LWANGA** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

## ...kuzindua sekondari iliyoathiriwa tetemeko

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. John Magufuli, leo anatarajiwa kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa chuo cha VETA Mkoa wa Kagera na kuzindua Shule ya Sekondari Ihungo, iliyojengwa upya baada ya kuathiriwa na tetemeko la ardhi Septemba, 2016.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, imesema Rais Magufuli ambaye ameongozana na mkewe Mama Janeth Magufuli, aliwasili mjini Bukoba jana akitokea Chato, mkoani Geita.

Akiwa njiani Rais Magufuli aliwasalimu wananchi wa Muleba na Kemondo na kuwashukuru kwa kumpigia kura nyingi katika uchaguzi mkuu uliomwezesha kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha pili.

Rais Magufuli amewahakikishia wananchi hao kuwa serikali itahakikisha ahadi zilizowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM (2020-2025) zinatekelezwa ili kuinua ustawi wa wananchi na kukuza uchumi wa taifa.

Alizitaka taasisi na mamlaka zote zinazohusika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa barabara, miundombinu ya elimu, afya na maji kutekeleza wajibu wao ipasavyo na kwamba yeye atafuatilia kwa ukaribu.

Aliwahakikishia wananchi wa Muleba kuwa barabara ya Kanyambogo – Nshamba (kilometa 5) itajengwa kwa kiwango cha lami, na kuagiza barabara ya Muleba – Rubya (kilometa 19) ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami, iitwe Barabara ya Mjungi (Mjungi Road) ikiwa ni kutambua mchango mkubwa wa Marehemu Mhandisi Leopord Mjungi, ambaye wakati wa uhai wake alisanifu na kusimamia ujenzi wa barabara nyingi nchini.

# JPM aagiza kuzalisha chakula kusaidia waathirika Covid-19

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli, amesisitiza umuhimu wa Watanzania kuzalisha kwa wingi mazao ya chakula, ili kuyasaidia mataifa ambayo hakuna uzalishaji kutokana na wananchi wake kufungiwa ndani kuepuka kusambaa kwa maradhi ya Covid-19 katika nchi zao.

Rais aliyasema hayo jana alipoungana na waamini wa Kanisa Katoliki la Bikira Maria wa Parokia ya Chato mkoani Geita kusali Misa Takatifu iliyoongozwa na Paroko, Padre Henry Mulinganisa.

Alisema Mungu ameiepusha Tanzania na corona, hivyo Watanzania wanapaswa kuitumia nafasi hiyo kuchapa kazi zaidi hasa kuzalisha mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula kwa ajili ya kuzisaidia nchi ambazo zinashindwa kufanya uzalishaji kutokana na watu wake kufungiwa majumbani na pia kukuza uchumi.

"Sasa hivi mvua zinanyesha katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, ninawaombeni sana ndugu zangu Watanzania, tulime mazao hasa ya chakula, tulime kwa wingi ili baadaye tuje kuwasaidia wenzetu ambao wanashindwa kulima kutokana na corona," Rais Magufuli aliagiza. Akitoa salamu katika misa hiyo, Rais Magufuli ambaye aliongozana na mkewe Mama Janeth Magufuli, alitoa wito kwa waamini hao na Watanzania wote kwa ujumla kuendelea kumtukuza na kumshukuru kwa baraka zake kwa taifa na hasa kwa kuwaepusha na janga corona ilhali ugonjwa huo unaendelea kusababisha vifo vya maelefu ya watu katika nchi nyingine duniani.

Pia, aliwapongeza waamini wa kanisa hilo kwa kufanikisha upanuzi wa kanisa lao ambalo sasa lina nafasi ya kutosha watu wengi zaidi na kufanya ibada kwa wakati mmoja.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene (kulia), akiweka jiwe la msingi la jengo la Utawala la kambi ya Boma Kichaka Miba, iliyopo wilayani Mkinga, Mkoa wa Tanga. Wanne kushoto ni Mkuu wa Mkoa huo, Martine Shigela, na watatu kushoto ni Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI.**

# Mbaroni tuhuma kuua babu yake katika mkasa wa ajabu

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

SAID Kihundwa (98), Mkazi wa Kijiji cha Mlangoni katika Kata ya Gararagua, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, anadaiwa kuuawa kikatili na mjukuu wake, aliyeona babu yake anateseka na maradhi kwa muda mrefu.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Leonard Makona, alithibitisha taarifa za kuuawa kwa mkazi huyo.

Tukio hilo lilitokea wiki iliyopita, majira ya jioni nyumbani kwa mzee huyo, mjukuu wake akidaiwa kumpiga na kitu kizito kichwani na kumsababishia umati.

Aliyekamatwa na anahojiwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma hizo ni Haruna Bashiru (27), Mkazi wa Kijiji cha Mlangoni.

Akifafanua zaidi kuhusu tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, John Mkanya, alidai mtuhumiwa wa mauaji hayo, alipokamatwa na askari wa Jeshi la Akiba (Mgambo) wa kijiji hicho muda mfupi baada ya tukio, alikiri kumpiga kichwani kwa kitu kizito babu yake Januari 11, mwaka huu.

Inadaiwa kuwa Kihundwa alikuwa akisumbuliwa na maradhi kwa muda mrefu na kwamba mjukuu wake Haruna, ambaye ndiye anatuhumiwa kwa mauaji, ndiye aliyekuwa akimuuguza.

Mkanya alisema kifo hicho kimeacha fumbo kubwa kwa familia ya Kihundwa na jamii kwa ujumla, kwa kuwa uamuzi wa mjukuu wa mzee huyo unaacha maswali mengi.

RIPOTI MAALUM

# Madereva wa mabasi, wenye hoteli kitanzini

## ■TAKUKURU yachunguza makubaliano yao
## ■LATRA, watetezi wa abiria watoa mwelekeo

**Na Elizabeth Zaya**

"UKIFIKA hotelini, kama huna fedha, utaishia kununua maandazi." Joackim Mwakalobo, mkazi wa Mbalizi mkoani Mbeya, analalamika kuhusu gharama kubwa za chakula kwenye hoteli zilizoko barabara kuu ya Tanzania-Zambia.

Mwakalobo anawasilisha malalamiko yake katika hali ya simanzi akisema: "Unawekewa chipsi kavu Sh. 3,000 na zinakuwa kidogo sana, tena za baridi na unaambiwa ulipie na cha kubebea Sh. 500.

"Hii ni kero kubwa kwetu sisi abiria wa mabasi ambao wengi wetu vipato vyetu ni vya kundunduliza. Mbaya zaidi, usiponunua kwenye hoteli yanakosimama mabasi, huna tena pengine pa kununua chakula.

"Ninafikiri kuna haja serikali kuweka bei elekezi kwenye hizi hoteli yanakosimama mabasi, ili kutatua tatizo hili linalochochewa na madereva ambao hotelini wanakula bure na wanapewa posho kwa kupeleka abiria kwenye hoteli husika."

Elina Kiwele, mkazi wa Dodoma, anaungana na Mwakalobo, akisema pamoja na vyakula kuuzwa kwa bei ghali, mazingira ya baadhi ya hoteli na migahawa yanakosimama mabasi, hayako katika viwango vinavyokubalika.

"Ukiingia chooni hata hamu kula inaondoka kutokana na uchafu uliokithiri huko," anasema Kiwele.




**KAULI YA TAKUKURU**

Huku kukiwa na malalamiko hayo yanayotoa ishara ya kuwapo viashiria vya rushwa na uonevu dhidi ya abiria, Nipashe inatua mezani kwa Ofisa Uhusiano wa Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU) Makao Makuu, Doreen Kapwani (pichani), kusaka majibu ya kinacholalamikiwa.

Katika majibu yake kwa gazeti hili, Kapwani anakiri taasisi hiyo kuwa katika uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazowakabili madereva wa mabasi na wamiliki wa hoteli na migahawa ya barabarani yanakopita mabasi ili abiria wake wapate huduma ya chakula na choo, maarufu 'kuchimba dawa'.

"Suala hilo tunalo tunalifanyia kazi. Tunaangalia kama huo utaratibu na makubaliano ya wenye hoteli na madereva wa mabasi yana viashiria vya rushwa," anasema.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la Mwaka 2004, inabainisha fasili ya neno 'rushwa' kuwa ni "fedha au kitu chochote cha thamani ambacho kinatolewa kwa mtu mwenye mamlaka ili mtoaji apewe upendeleo'.

Nipashe pia inahamia kwa Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA), ambacho Mwenyekiti wake Taifa, Hassan Mchangane, anasema malalamiko hayo ni ya muda mrefu.

Anasema kuwa wamekuwa wakizungumza na baadhi ya wamiliki wa mabasi na madereva kuhusu malalamiko hayo ya wateja, lakini hakuna jitihada zilizofanywa kutatua tatizo hilo.

"Hili ni tatizo la muda mrefu, na tatizo kubwa linasababishwa na hawa madereva na makondakta wao kupewa posho na kula bure kwenye hizo hoteli. Kwa hiyo, hawataki kusema ukweli japokuwa wanaujua.

Pia, baadhi ya hoteli hizo wanakopelekwa abiria kula, zinamilikiwa na baadhi ya wamiliki wa mabasi na ndiyo maana hata kama chakula au huduma ni mbovu, wanawapeleka tu bila kujali afya zao," anafafanua.

Mchangane anasema wanajipanga kupeleka andiko kwa mamlaka zote zinazohusika ili serikali itie mkono wake kushughulikia suala hilo.

**WAMILIKI MABASI**

Mustapha Mwalongo, Mkurugenzi wa Habari wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), anakiri kuwapo kwa malalamiko hayo na kubainisha kwamba utatuzi wake unahitaji mjadala mpana kwa kushirikisha wadau wote wanaohusika na sekta hiyo.

Kuhusu tuhuma za baadhi ya madereva kupewa fedha na wamiliki wa hoteli ili kupeleka abiria kupata huduma katika hoteli hizo, mkurugenzi huyo anakiri waajiriwa wao hao kufanya hivyo kwa migahawa na hoteli zenye hadhi ya chini.

"Hizo kamisheni wanapewa kwa hoteli za changanyikeni ambazo hazina wateja, na hizo ni zenye gharama ndogo ya chakula kuanzia Sh. 3,000 au 4,000, lakini hawawezi kufanya hivyo kwa zile zenye viwango vya juu," anabainisha Mwalongo.

Mkurugenzi huyo pia anakiri baadhi ya wamiliki wa mabasi kuwa na hoteli, hivyo huwapeleka abiria katika hoteli zao.

"Kuna baadhi ya mabasi hasa yenye hadhi kubwa, wamiliki wake wana hoteli pia, na ni za hadhi ya juu. Kwa hiyo, hawawezi kuwapeleka katika hoteli za changanyikeni.

"Ifike mahali hata abiria na wao kabla ya kukata tiketi, wawe wanauliza kwanza sehemu ambazo mabasi hayo yanasimama kula ili wajipime.

"Na ndiyo maana ninasema suala hili linahitaji mjadala mkubwa, kwa sababu hata abiria wenyewe hawatabiriki, unaweza kupeleka abiria wale katika hoteli A baadhi wakapenda na wengine wasipende. Ukiwapeleka hoteli B, wengine wanakubali baadhi wanakataa, labda serikali ijenge zake ndiyo itakuwa suluhisho," anasema.

**LATRA WAJIPANGA**

Udadisi wa Nipashe kuhusu mustakabali wa kero hiyo, unahamia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Johansen Kahatano, anayebainisha kwamba sheria na taratibu zinazosimamia sekta hiyo, hazitoi mwanya wa kudhibiti bei za vyakula.

"Kama tatizo hilo lipo, inabidi tukae chini tuangalie upya namna ya kufanya kulitatua hili kwa kuhusisha sekta zote tunazoshirikiana nazo katika hili," anasema.


**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**KUMB No. TATA/2020/DM/001**

**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** S.L.P 40780 Dar es salaam tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Ijumaa tarehe 29/01/2021 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai Mabatini.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T289DNT | DAR ES SALAAM |
| RAMADHANI MANENO MOHAMED | LP909 BUS | T810DMU | DAR ES SALAAM |
| NOBART JACOB MAGENI | LP 909 BUS | T343DPZ | MWANZA |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA: GSP AUCTION MART**
**PO BOX 310088 DAE ES SALAAM. +255 654 922 892, +255 687 638 679**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888, 40470
DODOMA,
12/01/2021.

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumanne tarehe 18/01/2021** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es salaam** kuelekea **Geita** gari hilo lenye namba za usajili: **T896DSD/T150CHN**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 18.0m**
   **Upana - mita 4.30m**
   **Kimo - mita 5.0m**
3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida,Tabora , Kahama hadi Geita Kupitia Bwanga**, ***gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



**KUMBUKUMBU**



**SIMON IVAMBI**

LEO TAREHE 18/1/2021 UMETIMIZA MIAKA ISHIRINI TANGU UITWE NA MWENYEZI MUNGU.
NI BIDII YAKO NA UZAZI MZURI AMBAO UMETUFANYA KUWA WATU TULIO LEO.
TUNAJARIBU KUISHI KAMA ULIVYO TUTUNZA NA KUTUFUNDISHA. LAKINI LEO HAUPO TENA KUONA MAENDELEO YETU. BABA, WEWE UKO MIOYONI MWETU NA KATIKA MAOMBI KILA WAKATI.
TUNAKUMBUKA UPOLE WAKO, UPENDO, BUSARA, HEKIMA NA MCHANGO WAKO MKUBWA WA USHAURI KATIKA FAMILIA.
PENGO ULILOLIACHA BABA YETU SIMON KAMWE HAKUNA WA KULIZIBA.
UNAKUMBUKWA SANA NA WANAO:
VERONICA, SEBASTIAN, OLIVA, JANETH NA FRIDA,
WAJUKUU ZAKO:HANS, LOUIS, MARTIN, AGATHA, SIMON SENIOR, BENARD, MARICELLA, SIMON JUNIOR, STEVIE, NANCY JUNIOR, NANCY SENIOR NA DIANA
DADA NA KAKA ZAKO, WAKWE ZAKO, SHEMEJI ZAKO , PAMOJA NA WANAFAMILIA WOTE NA WAUMINI WENZAKO.
DAIMA TUNAKUOMBEA BABA UPUMZIKE KWA AMANI

**BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA**
**JINA LA BWANA LIHIMIDIWE**

# Mauaji ya kutisha, kijana aua baba, dada naye auawa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MCHUNGAJI wa kanisa wilayani Nyamagana, jijini hapa na binti yake wameuawa kikatili kwa kuchomwa kisu na mtoto wake wa kiume ambaye naye alifariki baada ya kushambuliwa na wananchi wenye hasira. Mchungaji huyo wa Kanisa la Yesu Nakupenda Umeokoka, Beneth Karange (66) na binti yake Renatha Beneth (42), waliuawa juzi majira ya saa tisa alasiri.

Anayedaiwa kutekeleza mauaji hayo ni kijana wake wa kiume, Richmond Beneth, ambaye naye alifariki muda mfupi baada ya kufikishwa hospitali ya Sekouture, kutokana na kupigwa na wananchi wenye hasira. Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Murilo Jumanne, alisema Richmond (32), alikuwa akisoma Chuo Kikuu cha Kampala kilichopo jijini Dar es Salaam.

Kamanda Muliro alisema, kijana huyo ambaye naye aliuawa, aliwachoma kisu baba na dada yake sehemu mbalimbali za mwili na kusababisha vifo vyao papo hapo.

Muliro alisema kijana huyo aliyesababisha mauaji hayo, alirudi nyumbani kutoka chuoni kwa kukosa ada.

Alisema, kelele zilisikika nyumbani kwa mchungaji huyo na kusababisha wananchi kufika eneo la tukio na kumkuta muuaji akitoka na kisu huku akiwatishia kuwajeruhi, lakini walifanikisha kumkamata na kuanza kumshambulia kwa kumpiga na mawe na fimbo sehemu mbalimbali za mwili.

Alisema polisi walifika eneo la tukio na kumuokoa muuaji huyo kwa kumpeleka Hospitali ya Rufani ya Sekou Toure kwa matibabu, lakini alifariki muda mfupi baadaye.

"Inasikitisha kuona kijana huyu amemuua dada yake na baba yake, chanzo cha mauaji haya bado kinachunguzwa kwa kina, miili ya marehemu imehifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Sekou Toure," alisema Muliro.

Katika tukio lingine, lilitokea Januari 15, mwaka huu, wilayani Kwimba, Kijiji cha Mwabushana, Kata ya Maligisu, Lucas Mabula (54), alifariki dunia kwa kutumbukia kwenye mtaro wa maji na kusombwa na kwamba uchunguzi wa awali unaonyesha mtu huyo alikuwa akitembea bila kuchukua tahadhari barabarani.

# Wenyeviti kamati 14 za Bunge kujulikana leo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UCHAGUZI wa Wenyeviti na Makamu wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge 14 utafanyika leo, baada ya vikao vya kamati hizo kuanza, jijini hapa.

Huu ni mchuano mwingine bungeni kwa wabunge wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na wa upinzani ambao wanatarajiwa kupambana kuwania kuongoza kamati za Hesabu za Serikali (PAC) na Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), ambazo kwa mujibu wa kanuni za Bunge lazima ziongozwe na wabunge wa upinzani.

Ratiba ya kuanza vikao hivyo iliyotolewa na Ofisi ya Bunge jana, ilionyesha kuwapo kwa uchaguzi wa viongozi hao wa kamati 14.

Kamati zingine ambazo zitafanya uchaguzi huo mbali na PAC na LAAC, ni pamoja na Viwanda, Biashara na Mazingira, Katiba na Sheria, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Nyingine ni ya Utawala na Serikali za Mitaa, Huduma na Maendeleo ya jamii, Ardhi, Maliasili na Utalii, Kilimo, Mifugo na Maji, Miundombinu, Nishati na Madini, Sheria ndogo, Uwekezaji wa Mitaji ya Umma(PIC) na kamati ya Bajeti.

Wiki iliyopita taarifa iliyotolewa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge, ilisema kamati hizo zitakutana kutekeleza majukumu ya kibunge kuanzia leo hadi Januari 31, mwaka huu, kabla ya kuanza mkutano wa pili wa Bunge Februari 2, mwaka huu.

Pia, ilisema kwa muda huo kutakuwapo na mafunzo kwenye kamati mbalimbali ikiwamo ya majukumu na taratibu za uendeshaji wa kila kamati.

Mafunzo mengine ni kuhusu Bunge mtandao na usalama wa mtandao kwa kamati zote, kamati za kisekta kupokea maelekezo ya wizara kuhusu muundo, majukumu ya taasisi pamoja na sera na sheria zinazosimamiwa na wizara hizo.

Kadhalika, kutakuwa na mafunzo kwa Kamati ya PAC, LAAC, PIC na Bajeti kuhusu uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Msajili wa Hazina (TR) na namna bora ya kuhoji Maofisa Masuuli.

Kutakuwapo pia na mafunzo kwa Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo na uzoefu wa Mabunge mengine ya nchi zinazofuata mfumo wa kibunge wa Jumuiya ya Madola.

Katika taarifa hiyo, ilibainisha majukumu matano ya Kamati ya Bajeti katika kipindi hicho ikiwamo kupokea na kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka miaka mitano kuanzia 2021/22 hadi 2025/26.

Majukumu mengine ya kamati hiyo ni kupokea na kujadili taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa pili wa Maendeleo ya Taifa kwa miaka mitano 2016/17 hadi 2020/21.

Pia kupokea na kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka mmoja 2021/22, Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 na taarifa ya utekelezaji wa bajeti pamoja na Sheria ya Fedha kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2020/21.



Wafanyakazi wa Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar wakishusha shehena ya unga wa ngano ulioharibika kwa ajili ya kuuteketeza katika dampo la Kibele, Wilaya ya kati, Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Balozi Wright amuenzi mwanaharakati Martin Luther King

**Na Mwandishi Wetu**

MAREKANI leo inaadhimisha sikukuu ya kitaifa ya kumbukumbu ya kuenzi maisha ya urithi wa kinara mpigania haki za kiraia, mshindi wa tuzo ya Amani ya Nobel na mwanaharakati wa haki, usawa na utu wa mwanadamu, Martin Luther King, Jr.

Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Donald Wright, katika kuadhimisha siku hiyo, amesema watu duniani kote wanaifahamu hotuba mashuhuri ya "Nina ndoto" (I have a dream) aliyoitoa Martin Luther King mwaka 1963, akizungumzia matumaini yake ya watu wa rangi zote kuishi kwa amani na utangamano.

Balozi Wright katika salamu zake kupitia vyombo vya habari jana, alisema kiini cha hotuba hiyo iliyobeba ujumbe mzito kilikuwa ni tofauti kubwa iliyokuwapo kati ya ndoto aliyokuwa nayo Dk. King na hali halisi ya ubaguzi wa rangi iliyokuwapo nchini Marekani wakati huo.

"Kwa masikitiko makubwa, Dk. King aliuawa kabla ya kushuhudia ndoto yake ikitimia. Ni wazi kuwa hadi hivi leo, bado Marekani inahangaika ikikabiliwa na athari za muda mrefu za mifumo ya ubaguzi wa rangi, kama ambavyo dunia imeshuhudia katika tukio la mauaji ya George Floyd, mwaka jana," alisema.

Balozi Wright alisema Taifa la Marekani limejengwa katika imani kwamba binadamu wote waliumbwa wakiwa sawa na wana haki za kimsingi za binadamu ambazo hawawezi kutenganishwa nazo. Alisema katika maisha na kazi zake, Dk. King aliipa changamoto Marekani na kuitaka iishi kwa mujibu wa ahadi na maadili ya kimsingi ambazo taifa hilo limejengwa.

"Harakati hizi ni kitovu cha utambulisho wa Marekani. Utambuzi kwamba ahadi zetu bado hazijatimia umehamasisha kizazi baada ya kizazi kuchukua hatua za kupigania na kudai kupanuliwa kwa uhuru na usawa kwa watu wote, sio tu ndani ya Marekani, bali duniani kote."

"Kama tulivyoshuhudia hivi karibuni, demokrasia ya Marekani bado inaendelea kujengeka na kwamba ujenzi wake ni kazi inayoendelea kwamba demokrasia si kituo cha mwisho bali ni safari inayoendelea. Jitihada na urithi wa Martin Luther King zinatukumbusha kuwa kila wakati ni wakati sahihi wa kufanya jambo sahihi."

Alisema Marekani haiwezi kuogopa au kukataa kupaza sauti dhidi ya ukiukwaji wa haki. Badala yake, kukubali upungufu wake na kuendelea kupigania misingi wanayoiamini ya uhuru na usawa kwa wote na kuendelea kusimama pamoja na wale wanaoamini katika misingi hiyo, ikiwamo Tanzania.

"Ni kwa sababu hiyo, tunaendelea kuchagiza pawapo na maendeleo zaidi na kuenzi kumbukumbu ya Martin Luther King," alisema.

# Polisi watakaoshindwa kudhibiti wahamiaji haramu kutumbuliwa

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ameonya kuwa polisi watakaoshindwa kuwabaini wahamiaji haramu hususani maeneo ya mipakani wanapoingilia, watawajibishwa.

Waziri Simbachawene alieleza kuwa kitendo cha wageni hao kukamatwa maeneo mbalimbali ndani ya nchi wakiwa wameshavuka mipaka ni kutokana na kuwepo na mawakala wanaofanikisha wahamiaji hao kuingia nchini.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo ya uongozi kwa maofisa na askari wa Idara ya Uhamiaji katika kambi mpya ya mafunzo ya Boma Kichaka Miba iliyopo wilayani Mkinga, Mkoa wa Tanga, aliwaambia watawashughulikia askari wote wanaokaa katika mikoa ya mipakani ambayo wahamiaji hao wanaingia kwa mara ya kwanza.

"Wahamiaji haramu kama tukiwakuta Morogoro na wakasema wameingia hapa Mkinga, sisi hatushughuliki na wale Morogoro, tutashughulika na waliopo wilayani Mkinga na Tanga, tuwahoji wamepitajepitaje ...," alisema Simbachawene.

Aliongeza: "Pia tutawauliza polisi, ilikuwaje msiwaone wahamiaji hawa haramu maana 'barrier' zote zenu, hawa hawatembei kwa miguu, walipanda gari, walipandia wapi gari, na kama wakituambia walipanda gari, hawa watu wote (polisi na uhamiaji) wapo kwenye wizara yangu, wote nitawafagia." Pia alisema mipaka lazima ilindwe kwasababu askari wanataaluma zote za kijeshi ya kupambana na wahamiaji haramu hivyo kitendo cha kupita mipakani na kukamatwa maeneo ya ndani ya nchi ni hatari na kama adui atakuwa amelishambulia taifa.

Ukiona msafara wa wahamiaji haramu umefanikiwa kutoka 'point A mpaka B' ujue kuna mawakala, kutoka sehemu B mpaka C wapo mawakala, wanaokuja ni wageni, wanawezaje kupita point A mpaka B, kama wamefanikiwa kufika mpaka Dar es Salaam wakakamatwa Tegeta au Mbezi, maana yake tumeshapigwa kama ni adui, lazima tuwe makini kila mtu katika eneo lake," alisema Simbachawene.

Vivile, aliwataka wanafunzi wa kambi hiyo kuzingatia masomo ya Kiuhamiaji wanayopewa yakiwemo ya uongozi na utawala, masuala ya kikonsula, mawasiliano, ulinzi wa kujihami na gwaride. "Mafunzo mtakayoyapata kutoka kwa wakufunzi wenu yanalenga kudumisha nidhamu ya kijeshi, uzalendo, utii, uwajibikaji na maadili bora, ninawaomba zingatieni tunu hizo katika kipindi hiki chote cha mafunzo, kwani ndiyo silaha kubwa kwa askari na katika uongozi bora," alisema Simbachawene.

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji (CGI), Dk. Anna Makakala, alisema mafunzo katika kambi huyo mpya, yanajumuisha askari na maofisa wa uhamiaji 287, wanawake 81 na wanaume 206.




Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo (watatu kushoto), akimsikiliza Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Gilbert Mvungi (wanne kushoto), akimpa maelezo ya chanzo cha maji kinachoonekana pichani kinachotumika wakati wa tukio la kuzima moto na uokozi wakati wa ziara ya kikazi ya naibu waziri huyo kutembelea Makao Makuu ya jeshi hilo, leo jijini Dodoma. **PICHA NA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

## Muuguzi, Sungusungu mbaroni tuhuma kuiba dawa zahanati

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MUUGUZI wa Zahanati ya Kijiji cha Nyamalogo, wilayani Shinyanga, William Desdez na askari wa Sungusungu Fedson Matekele, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa kwa tuhuma za wizi wa dawa kwenye zahanati hiyo.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, akitoa taarifa hiyo jana kwa vyombo vya habari, alisema tukio hilo lilitokea Januari 12, mwaka huu, baada ya kuwapo na taarifa kuwa kuna dawa za binadamu zinauzwa nyumbani kwa Matekele, na kufika nyumbani hapo na kuzikamata.

Alisema walipofika nyumbani kwa mtuhumiwa huyo, walizikuta dawa hizo zikiuzwa na walipozichunguza waligundua kuwa zimeibwa kwenye zahanati ya kijijini na mhusika mkuu ni muuguzi wa zahanati hiyo Desdez. Watuhumiwa wote wanashikiliwa kwa uchunguzi zaidi.

"Dawa zilizoibwa baadhi yake zimeshakwisha muda wa matumizi, lakini zimekuwa zikiuzwa kwa wananchi na kuendelea kuzitumia, hali ambayo ni hatari kwa afya zao, na uchunguzi utakapokamilika watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani," alisema Magiligimba.

Kamanda aliwataka wananchi mkoani humo, kuendelea kutoa taarifa kwa jeshi hilo matukio ya uhalifu, ili wahusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua kazi za kisheria.

# Nyama ya 'kitimoto' yapigwa marufuku wilayani Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamringi Macha, amepiga marufuku uuzwaji wa nyama ya nguruwe maarufu 'kitimoto' baada ya kuibuka ugonjwa wa homa kali iliyosababisha vifo 500 vya wanyama hao.

Macha alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake, wakati akitoa taarifa ya kuingia kwa ugonjwa wa homa kali ya nguruwe (African Swine Fever), wilayani humo mwishoni mwa mwezi uliopita.

Alisema amechukua uamuzi huo ili kuwakinga wananchi wanaotumia nyama hiyo hadi serikali itakapojiridhisha kuwa ugonjwa huo umetoweka.

Alifafanua kuwa dalili za ugonjwa huo zilianza kujitokeza kipindi cha mwezi Desemba hadi Januari 2021 na unaendelea kusambaa na kushauri biashara hiyo kusitishwa ili kuepusha bmadhara kwa wananchi.

Macha alisema zaidi ya nguruwe 500 katika mazizi matano ya wafugaji wa wanyama wilayani hapo wamekufa kwa kipindi kifupi kutokana na ugonjwa huo na moja ya dalili ni nguruwe kukosa hamu ya kula, mimba kutoka, kuwa mwekundu sehemu za masikio na mdomoni na kushindwa kupumua, hatimaye kufa.

Alisema lengo la serikali ni kuzuia kusambaa kwa maambukizi hayo kwenda mikoa mingine na wilaya jirani kutokana na ugonjwa huo kutokuwa na chanjo wala kinga, huku akitaja chanzo cha ugonjwa huo.

"Hatutaki tusikie ugonjwa huo umeingia mkoa jirani ukitokea Kahama, ombi langu ni kwamba wananchi kama wataona mtu yeyote anasafirisha nguruwe kupitia toroli ama gari mtoe taarifa kwenye uongozi wa maeneo yao ili hatua zichukuliwe dhidi ya watu hao," alisema Macha.

Alipiga marufuku usafirishaji wa wanyama hao kutoka sehemu moja kwenda nyingine bila kibali cha daktari, huku akiwataka wafugaji kuepuka vishoka wanaojiita madaktari na atakayebainika kukiuka agizo hilo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Ofisa mifugo wa Halmashauri ya mji wa Kahama, Dk. Damian Kilyenyi, alithibitisha kuwapo kwa ugonjwa huo na zaidi ya nguruwe 500 wamekufa mpaka sasa.

Aliwataka wafugaji na wafanyabiashara kuweka wanyama hao sehemu moja mpaka watakaporuhusiwa kufanyabiashara ili kuzuia kuendelea kusambaa kwa ugonjwa huo.

Salvatory Moshi, miongoni mwa wafanyabiashara wa nguruwe, alipongeza hatua ya serikali ya kuzuia biashara hiyo mapema kabla ya ugonjwa huo haujasambaa na kwamba atahakikisha anafuata maelekezo yaliyotolewa na serikali.

Wakati huo huo, Macha ametangaza vita na wazazi wote watakaoshindwa kuwapeleka watoto wao shule waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa kisingizio cha kukosa mahitaji ya shule.

Alisema, mzazi atakayebainika kutompeleka mtoto shuleni na anamiliki mifugo kama ng'ombe, mbuzi au kondoo atawauza mmoja kwa njia ya mnada na fedha itakayopatikana itatumika kununua mahitaji ya mwanafunzi na itakayobaki atarejeshewa mzazi.

Alisema, serikali itawachukulia hatua za kisheria wazazi wote watakaobainika kuwazuia watoto wao hasa wa kike waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenda shule kwa kipindi hiki cha ukaushaji wa zao la tumbaku ambalo asilimia kubwa linahitaji vibarua wengi.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Taifa Stars anzeni kwa ushindi CHAN

**BAADA** ya Jumamosi kushuhudiwa wenyeji Cameroon wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Zimbabwe kwenye mechi ya ufunguzi wa michuano ya Fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), huku siku hiyo Mali nayo ikipata ushindi kama huo dhidi ya Burkina Faso, kesho ni zamu ya Taifa Stars dhidi ya Zimbia.

Mechi hiyo ya Taifa Stars na Zambia ni ya saba katika michuano hiyo tangu ifunguliwe Jumamosi, baada ya kushuhudiwa pia Libya na Niger zikimenyana, DR Congo wakipepetana na ndugu zao Congo, Morocco ikichuana na Togo pamoja na Rwanda wakitoana jasho na Uganda.

Mbali na Zambia kundi hilo la Stars pia linazijumuisha Guinea na Namibia, ambazo nazo zitashuka dimbani kesho kukamilisha raundi ya kwanza ya michuano hiyo ambayo imepangwa katika makundi manne.

Katika kundi hilo, Zambia ndiyo timu inayoonekana kuwa tishio zaidi, hivyo kama Taifa Stars itapata matokeo kesho itakuwa imejiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kupenya hatua inayofuata ambayo ni robo fainali.

Tunaamini maandalizi yaliyofanywa na Taifa Stars chini ya Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, yanatosha kuweza kuibuka na ushindi kama wachezaji watafuata vema maelekezo yake huku wakijituma na kujitoa mwanzo mwisho kwa kutanguliza mbele thamani ya kuaminiwa kuvaa jezi ya taifa.

Mbali na kila mchezaji kutakiwa kuonyesha uwezo binafsi lakini pia kucheza kitimu ni silaha nyingine itakayoweza kuibeba Taifa Stars hususan dhidi ya vigogo hao wa soka Afrika, Zambia.

Kila mchezaji hana budi kuona ushindi ndio kila kitu katika mechi hiyo ya kwanza ya kundi lao, kwani endapo Stars itapata matokeo kwenye mechi hiyo, utachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza morali katika mechi zinazofuata na kuifanya kujiweka mazingira mazuri ya kutinga robo fainali.

Ni wazi haitakuwa mechi rahisi kwa kila upande, lakini wachezaji wa Taifa Stars hawana budi kutambua kwamba mbali na malengo yao ya kupeperusha vema bendera ya nchini kimataifa, pia huu ni wakati wakutangaza vipaji vyao na kuviweka sokoni.

Nipashe tunatambua mawakala wengi wanaitupia jicho CHAN ili kupata wachezaji wakuwauza katika klabu mbalimbali ndani na nje ya bara la Afrika, hivyo ni wakati wa kila mchezaji kujituma mwanzo mwisho ili kuitumia michuano hiyo kama daraja la kufikia malengo yao ya kucheza soka la kulipwa.


Tunaamini kila mchezaji ndoto zake ni kucheza soka la kulipwa Ulaya na kwingineko barani Afrika kulikopiga hatua kisoka, hivyo hii ni fursa adimu ambayo wachezaji wengi hususan wa nchi za Magharibi wamekuwa wakiitumia kama daraja lao la kwenda kucheza Ulaya, jambo ambalo linapaswa kuigwa pia na nyota wa Taifa Stars.

Katika soka hakuna njia ya mkato ya kufikia malengo zaidi ya kuonyesha uwezo dimbani husuan kwa wachezaji wanaopata fursa kama hii ya kucheza michuano hiyo ya pili kwa ukubwa barani Afrika kwa ngazi ya timu za taifa baada ya ile ya Afcon.

Matarajio na maombi yetu si tu kuona Taifa Stars ikitinga robo fainali, nusu na hata fainali kama si kuubeba ubingwa huo, bali pia tunataka kushuhudia wachezaji wengi wakipata nafasi ya kucheza soka la kulipwa Ulaya na kwingineko Afrika kupitia vipaji vyao kuonekana kwenye michuano hiyo.

Hivyo, tunaitakia kila la kheri Taifa Stars katika mwanzo mwema wa michuano hiyo na mechi zinazofuata kwenye michuano hiyo ambayo hii ni mara ya pili kwa Tanzania kushiriki baada ya 2009 kushiriki kwa mara ya kwanza na kuishia hatua ya makundi nchini Ivory Coast.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






# Muungwana Lazima Nilonge

## Kila la kheri Taifa Stars CHAN kesho

Na Adam Fungamwango

**AMEBAKI** mchezaji mmoja tu ambaye alikuwa yupo kwenye michuano ya Fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) iliyofanyika nchini Ivory Coast mwaka 2009 kuanzia Februari 22 hadi Machi 8. Si mwingine ni Erasto Nyoni.

Wengine wote 22 hawapo tena kwenye kikosi hicho, ingawa baadhi yao wanaendelea kucheza Ligi Kuu Tanzania, wengine wameshakuwa makocha na baadhi wameshataafu kabisa kucheza soka.

Imekuwa ni rekodi ya ina yake kuwa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars inarejea tena CHAN baada ya miaka 12, ikiwa na mchezaji ambaye pia alikuwapo kwenye kikosi hicho.

Mara ya kwanza kilikuwa chini ya Mbrazil Marcio Maximo, lakini safari hii kimekwenda nchini Cameroon kikiongozwa na Mrundi Etienne Ndayiragije. Kesho kikosi hicho kitatupa karata yake ya kwanza kwa kucheza dhidi ya Zambia kesho.

Ikumbukwe kuwa hata mwaka 2009, Stars ilikuwa kundi moja na Zambia na katika mechi yao ya Kundi A zilitoka sare ya bao 1-1, bao la Stars likifungwa na Shadrack Nsajigwa, hivyo kesho ina sababu zote za kuweza kuifunga Zambia na kujiwekea mazingira mazuri ya kusonga mbele kwenye Kundi lao D zikiwa pamoja na Guinea na Namibia.

Ukiliangalia kundi hili si la kutisha sana kama wachezaji wa timu hiyo wataamua kupambana, tofauti na lile la miaka 12 iliyopita lililokuwa na Zambia, Senegal na Ivory Coast.

Mara nyingi kwenye michuano kama hii ya makundi, ni vizuri zaidi kushinda mechi ya kwanza.

Ni mechi ambayo inawajengea wachezaji kujiamini, lakini pia pointi tatu zinazopatikana zinaifanya timu kuanza mahesabu yake kwenye mechi mbili zilizobaki, kama moja itoke sare yoyote vile, lakini inapopoteza inabidi kupambana ili kushinda mechi zote mbili kwa lazima.

Halafu pia hapo hapo linakuja lile suala la kuanza kuomba timu fulani ipoteze. Kitakachoibeba zaidi Stars kwenye michuano hii ni kwamba ina wachezaji wake wengi ambao ndiyo hao hao wanaunda timu ya jumla ya Taifa Stars ambayo inawajuisha pia wachezaji kutoka nje ya nchi.

Tunajua kuwa baadhi ya nchi zinazoshiriki michuano hiyo, huwa wanaita wachezaji zaidi ya asilimia 90 kama si 100 wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi, wakati mwingine hata wachezaji wa akiba watakuwa ni wa nje ya nchi.

Linapokuja suala la michuano ya ndani ya nchi wanakuwa na wachezaji ambao viwango vya havitishi sana. Hii ni tofauti na Taifa Stars, ambayo haina hata wachezaji 10 wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi na mara nyingi tegemeo linakuwa kwa Mbwana Samatta na Simon Msuva tu, lakini mara nyingi wengi wanakuwa ni wale wale wanaocheza soka ndani ya nchi.

Kwa maana hiyo nataka kusema kuwa nchi nyingi kwenye CHAN zinaweza kuwa na kisingizio kuwa zilikosa wachezaji wanaocheza soka nje ya nchi yao ndiyo maana hawakufanya vema kwa sababu hao ndiyo wanawategemea zaidi, lakini si kwa Stars.

Yenyewe hata kwenye kikosi cha jumla cha Stars kinatumia asilimia 90 ya wachezaji wa ndani, na kwa asilimia kubwa ndiyo hao hao ambao wako CHAN.

Huu ni wakati wa kuithibitishia Afrika na dunia kuwa kwa sasa Tanzania kuna vipaji ambavyo vinapaswa kumulikwa. Ni wakati vile vile kwa wachezaji wa Kibongo kujiunza kwani mara nyingi michuano hiyo, inakuwa imejaa mawakala kutoka nchi mbalimbali duniani.

Kuwapo kwa wachezaji wa kigeni wanaocheza soka kwenye Ligi ya Tanzania, pia kumesababisha wachezaji wa Kibongo kutokuwa na hofu sana wanapocheza na timu za kigeni tofauti na zamani ambapo walikuwa wanacheza wenyewe kwa wenyewe na wanakuwa wamezoeana.

Wanapokutana na wachezaji wa kigeni, wachezaji wengi walikuwa wana wasiwasi sana, lakini kwa sasa hilo halipo. Tunawatakia kila la kheri Taifa Stars kufanya vema kwenye michuano hiyo ya CHAN kuanzia mechi ya kesho dhidi ya Zambia na zinazofuata pia.

## Waomba kujengewa kivuko cha uhakika

**Na Idda Mushi,** MLIMBA

WANANCHI wa vijiji vya Mngeta na Isango, Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, wilayani Kilombero, wameiomba serikali kuwajengea daraja au kivuko cha uhakika kwenye Mto Mngeta cha kuunganisha vijiji hivyo kutokana na kutegemea mtumbwi wa mtu binafsi.

Walisema hali sio salama katika mto huo kutokana na kujaa mamba ambao hujeruhi watu na kusababisha vifo kwa baadhi yao.

Wakizungumza na Mwandishi wa habari hizi katika maeneo ya mto huo, baadhi ya wananchi, Angelina Soma wa Kijiji cha Isango na Agnes Chawana wa Mngeta, walisema usafiri huo wa mtumbwi ni kero kubwa kutokana na mmiliki wake kufunga huduma saa 12 kamili jioni, hali inayowalazimu kuahirisha shughuli zao zikiwamo za kilimo.

"Huwa tunatozwa shilingi mia tatu kwa kichwa, kama una baiskeli unatozwa mia tano, na wanafunzi huwa ni bure, lakini usafiri huu sio wa uhakika kutokana na muda wake na hatari ya mamba waliojaa kwenye mto huu," alisema Soma.

Walibainisha kuwa vijiji hivyo vina huduma muhimu kama zahanati, shule ambazo zinalazimu kuvuka upande mmoja kwenda mwingine.

Walidai wakati mwingine wananchi wakichelewa kuvuka, hulazimika kupiga mbizi kuvuka mto huo, hali inayo hatarisha maisha yao kutokana na mamba kuwapo kwenye mto huo.

Vile vile, walidai barabara ya kutoka Ifakara Mlimba kufika kwenye vijiji vyao ni mbovu na shida zaidi hujitokeza wakati wa mvua kutopitika.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mngeta, Clifford Mnewa, alisema tatizo kubwa hujitokeza majira ya usiku wakati wanapopata mgonjwa au mjamzito anayetaka kujifungua na kivuko kutofanya kazi ya kutoa huduma.

Mbunge wa Jimbo la Mlimba, Godwin Kunambi, akizungumza na wananchi wa pande zote mbili, baada ya kuvuka kutoka Isango kuingia Mngeta kwa kutumia mtumbwi huo, alisema serikali inafahamu kero hiyo na imeanza kuchukua hatua kukabiliana nayo.

"Serikali inakusudia kujenga kwanza daraja la muda la mbao kuwezesha wananchi kuvuka, wakati tukisubiri mikakati ya kuhakikisha kunakuwa na daraja la kudumu," alisema Kunambi ambaye hivi karibuni aliwezesha pia kujengwa daraja jingine la muda kuunganisha Kijiji vya Tanganyika na maeneo mengine ya kata na wilaya hiyo baada ya daraja la sasa kuoza na kushindwa kupitisha magari.

Kunambi alisema, anaendelea kutatua vipaumbele vya wananchi kwa kila kata kwa kuhakikisha zote 16 za halmashauri hiyo zinakuwa na kituo cha afya na kuongeza kasi ya madarasa ili wanafunzi wote waliofaulu waendelee na kidato cha kwanza.



Mkuu wa Chuo cha Kijeshi cha Sayansi ya Tiba cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Brigedia Jenerali Charles Mwanziva, akimpongeza mmoja wa wahitimu wa fani ya ofisa tabibu wakati wa mahafali ya pili yaliyofanyika chuoni hapo Lugalo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadaiwa pango ardhi kunyang'anywa viwanja

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka watumishi wa sekta ya ardhi katika Mkoa wa Arusha wanaodaiwa kodi ya pango la ardhi kulipa kodi hiyo vinginevyo watanyang'anywa viwanja wanavyomiliki kama inavyofanyika kwa wananchi wasio watumishi.

Akizungumza hivi karibuni mkoani Arusha na watendaji wa sekta ya ardhi katika mkoa huo akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi wa sekta ardhi, Dk. Mabula aliwataka wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Arusha kuandaa orodha ya watumishi wanaodaiwa kodi ya ardhi na kumpatia ili aweze kuwafuatilia na kusisitiza kuwa kwa wale watumishi watakaoshindwa kulipa kiasi wanachodaiwa watanyang'any wa viwanja vyao. "Wakurugenzi, watumishi wenye viwanja na ambao hawajalipa kodi ya pango la ardhi nataka nipate orodha yao, na watakatwa kwenye mishahara yao maana ni deni kama yalivyo madeni mengine, kama huwezi kulipa kubali tuchukue kiwanja chetu au ukubali tuchukue pesa yetu," alisema Dk. Mabula.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, wizara yake katika ufuatiliaji wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi haiangalii mashirika, taasisi, kampuni au watu binafsi pekee bali inaangalia pia watumishi wa umma aliowaeleza kuwa wakati wakichukua viwanja walifahamu kama wanapaswa kulipa kodi ya pango la ardhi.

Akigeukia Taasisi za Umma zenye madeni makubwa ya kodi ya pango la ardhi, Dk. Mabula alisema mpango wa kulipa madeni hayo kwa taasisi hizo umeshawekwa ikiwamo kuwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali namna ya kuzibana taasisi za umma na kusisitiza kuwa kwa zile ambazo zimeonyesha nia ya kulipa ziendelee kukamilisha madeni yao ili kuepukana na mkono wa sheria.

## Magereza waokoa bilioni 11/- chakula cha wafungwa

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Magereza limeokoa Sh. bilioni 11, zilizokuwa zinatumika kununua chakula cha wafungwa, baada ya kuanza kuzalisha kwa kutumia nguvu kazi iliyoko magerezani.

Jeshi hili lilikuwa linatumia wastani wa Sh. bilioni moja kwa mwezi kulisha wafungwa magerezani. Hatua za kujitegemea kwa chakula ni maelekezo ya Rais John Magufuli, ya kutaka jeshi hilo litumie nguvu za wafungwa kuzalisha chakula.

Akizungumza katika makao makuu mapya ya jeshi hilo yaliyoko Msalato jijini Dodoma, Kamishna Jenerali wa Magereza, Suleiman Mzee, alisema walikuwa wanatumia bilioni moja kila mwezi kulipa wazabuni wa chakula waliokuwa wanaliuzia chakula jeshi hilo. "Hivi sasa tunajitegemea kwa chakula kwa asilimia kubwa, kabla ya Machi mwaka jana kila mwezi jeshi lilikuwa na deni la bilioni moja za ununuzi wa chakula, lakini baada ya mwezi huo wa tatu sasa tunaokoa kiasi hicho cha fedha na mpaka sasa tuna miezi 11 tunajilisha wenyewe kupitia shirika la Magereza" alisema CGP Mzee

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Naibu Waziri, Khamis Chilo, alilipongeza Jeshi la Magereza kwa kutekeleza vyema agizo la Rais Magufuli, pamoja na kujenga kiwanda kikubwa cha samani ambacho mpaka kukamilika kwake kitagharimu Sh. bilioni 1.1.

"Niwapongeze kwa hatua mbalimbali za maendeleo ambazo nimeshuhudia mwenyewe, lakini kubwa kuweza kujitegemea kwa chakula cha wafungwa hali iliyookoa kiwango kikubwa cha fedha ambacho sasa mnakitumia kwa shughuli nyingine za maendeleo hongereni sana" alisema Naibu Waziri.

## Bil. 74/- kuboresha mafunzo ya DIT

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

CHUO cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT), kinatarajia kutumia takribani Sh. bilioni 74 kuboresha mafunzo ya ufundi kwenye sekta za mawasiliano na ngozi.

Lengo ni kufanikisha mpango wa serikali wa kukuza viwanda na kufikia uchumi wa kati, ikifafanuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Profesa Maulilio Kipanyula, aliyebainisha hayo wakati wa mahafali ya DIT Kampasi ya Mwanza mwishoni wa wiki.

Aliongeza kuwa mradi huo wa miaka mitano unalenga kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ili kufikia mageuzi ya ufundishaji.

Alisema mradi huo pia unalenga kuboresha mafunzo ya ufundi yanayohitajika katika soko la ajira katika Ukanda wa Afrika Mashariki, ili kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. "Mradi huu unagharamiwa na serikali kupitia mkopo wa Benki ya Dunia (WB). Utaiwezesha DIT kutambulika kikanda kwa umahiri wa uendeshaji wa mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA) na usindikaji ngozi," alisema Professa Kipanyula.

Aidha, alisema DIT inatekeleza mradi mwingine wa Shilingi bilioni 33 wa kuendeleza ajira na elimu ya ufundi, unaolenga kuisaidia taasisi hiyo kujitegemea na kuendesha mafunzo ya ufundi kwa ufanisi ili kuzalisha wataalamu wanaoajirika au kujiajiri.

Mkuu wa Taasisi ya DIT, Professa Preksedis Ndomba, alisema wanafunzi 18 walihitimu stashahada ya sayansi na teknolojia ya maabara na kwamba mafunzo hayo yalijikita kwa vitendo na ziara kwenye maabara na viwanda.

Alisema mfumo huo unazalisha wataalam waliobobea katika ufundi, ubunifu na ujasiriamali unaowawezesha kujiajiri.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kapole, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliwataka wahitimu hao kutumia elimu waliyoipata kutatua changamoto zinazowakabili pamoja na jamii.

Alisema serikali imelenga kuanzisha viwanda vidogo vya kati na vikubwa na kuvifufua visivyo na ufanisi ili kuongeza thamani ya bidhaa ambazo nyingi huuzwa nje ya nchi zikiwa ghafi.

# Zimamoto yakusanya mabilioni tozo ukaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limekusanya jumla ya Sh. Bilioni 81.337 katika kipindi cha miaka mitano ikiwa ni gharama za ukusanyaji wa tozo za ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto katika majengo 356,845 nchini.

Majengo hayo ni viwanda, hoteli, shule, masoko, migodi, maduka, hospitali, ofisi, matangi ya mafuta, nyumba za kuishi na vyombo vya usafiri.

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John Masunga, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya jeshi hilo kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, wakati wa ziara ya kikazi makao makuu ya jeshi hilo, jana jijini Dodoma. "Kwa kuwa ukaguzi huo wa kinga na tahadhari ya moto huenda sambamba na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali, jeshi limefanikiwa kukusanya jumla ya Sh. 81,336,956,451, Jeshi la Zimamoto linaendelea na jitihada za kuboresha maduhuli ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa mfumo mpya wa makusanyo ambao utasaidia kupunguza upotevu wa maduhuli ya serikali," alisema Kamishna Masunga.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Chilo alilipongeza jeshi hilo huku akilitaka liongeze ufanisi ikiwamo kufika haraka katika matukio ya moto ili kunusuru maisha na mali za wananchi.

"Kumekuwapo na malalamiko juu ya askari wetu kuchelewa kufika katika maeneo ya moto au ajali yoyote ili kufanya maokozi, nawasihi kufika haraka katika matukio mbalimbali kwa kuwa wananchi wanawategemea na uwapo wenu unasaidia mambo mengi kwa kuwa nyie ndio mna utaalamu na udhibiti wa majanga ya moto na uokozi," alisema.

Jeshi hilo pia limefanikiwa kukamilisha ujenzi wa jengo la makao makuu jijini Dodoma, Kituo cha Zimamoto na Uokoaji katika Wilaya ya Chato, mkoani Geita, linaendelea na ujenzi wa kituo cha zimamoto wilayani Chamwino na ujenzi wa nyumba za askari wake katika eneo la Kikombo, jijini Dodoma.



Naibu Waziri Kilimo, Hussein Bashe, akiongea na Wakulima wa Skimu ya Mwamalili katika Hamashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini alipofika kuitembea na kukagua shughuli za skimu hiyo yenye ukubwa wa hekari 5,000 ambayo imesimama kwa sasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti malipo kampuni za madini na gesi yakamilika

**Na Rose Jacob,** MWANZA

TAASISI ya Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative (TEITI), imekamilisha ripoti 10 za takwimu za malipo ya kampuni za madini na gesi asilia kwa kipindi cha mwezi Julai mwaka 2008 hadi Juni mwaka 2018.

Akisoma taarifa ya utendaji kazi wa TEITI, mbele ya Naibu Waziri wa Madini, Profesa Shukrani Manya, Mwenyekiti wa TEITI, Ludovick Utouh, alisema kazi hiyo imeshakamilika.

"Maandalizi ya ripoti hii ambayo imesababisha serikali kukusanya kiasi cha Dola za Marekani bilioni 3.51, yalitanguliwa na kazi ya uchambuzi wa kampuni zinazojishughulisha na uchimbaji wa madini, utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kipindi cha Julai 1, mwaka 2017 hadi Juni 30, mwaka 2018," alisema Utouh.

Utouh alisema kunahitajika kuweka wazi malipo ya kodi kutoka kwenye kampuni za uzinduaji na mapato yaliyopelekwa serikalini ili kuhamasisha uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia.

Naye Naibu Waziri wa Madini, profesa Manya, aliwataka wachimbaji wadogo nchini kuacha kutorosha madini na badala yake wafanye shughuli zao kwa kufuata sheria na utaratibu uliowekwa ili kuiwezesha nchi kuongeza mapato.

"Tuendelee kuwasihi wachimbaji wadogo kufanya maisha ya wizara inayowasimamia kuwa mepesi kwa kuacha kutorosha madini," alisema.

Aliwataka wahusika wote wa sekta ya madini kuacha tabia ya kukaa kimya kwenye vikao na kutimiza wajibu wakuchangia mada ya uelimishaji wa madini, gesi asilia na utafutaji wa mafuta kwa kuwa nchi imewaamini.

HABARI KITAIFA

## Mwenyekiti UVCCM ataja ujenzi nyumba za makada

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Kheri James, amesema lengo la chama hicho kujenga nyumba za makatibu wake ngazi ya mkoa na wilaya, ni kuhakikisha wanaondokana na kero za nyumba za kupanga, ikiwamo ulipaji kodi, pamoja na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akifungua nyumba ya Katibu wa UVCCM Mkoa wa Kilimanjaro, Safina Nchimbi, iliyogharimu Sh. milioni 48 na kusema lengo la kujengwa kwa nyumba hizo ni kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Alisema deni kubwa limebaki kwa watendaji watakaoishi katika nyumba hizo, kuzitunza ili ziweze kudumu muda mrefu pamoja na kuwatia moyo wale wote waliojitolea michango yao kufanikisha ujenzi.

Mwenyekiti huyo alisema UVCCM ndiyo jumuiya imara na kongwe ya CCM ambayo ina historia kubwa ya kutoa viongozi wengi ambao wameonyesha utendaji kazi uliotukuka.

Alisema vipo vyama vya siasa nchini ambavyo havina majengo ya ofisi ya taifa, lakini UVCCM unajenga nyumba za kuishi watendaji wake.

"Umoja wa vijana ni tanuru la kuoka viongozi, hivyo ujenzi wa nyumba hizo ni kuonyesha jinsi gani viongozi hao wataweza kusimamia miradi ya maendeleo ya wananchi pindi watakapopata nafasi za kuongoza," alisema James.

Alisema katika kanda ya Kaskazini Mkoa wa Kilimanjaro, umekuwa wa kwanza katika kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Katibu na kueleza kuwa Mwenyekiti wa UVCCM, Mkoa wa Kilimanjaro, Ivan Moshi, amedhihirisha ana uwezo wa kusimamia miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Kilimanjaro, Ivan Moshi, alisema matokeo makubwa yanasababishwa na uamuzi magumu na kudai kuwa nyumba hiyo imejengwa kupitia michango mbalimbali ya wananchi na wanachama wa CCM.

Alisema UVCCM Mkoa wa Kilimanjaro wanamiliki eneo la ukubwa wa hekari tatu, lakini halizalishi kutokana na kukosa mwekezaji na walimuomba James kuwatafutia wawekezaji.

# Muuguzi aliyemzaba makofi mjamzito afunguka

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

CHAMA cha Wauguzi Tanzania (TANNA), Baraza la Wauguzi, wanatarajia kukutana kuangalia sheria, kanuni pamoja na adhabu atakayostahili muuguzi anayedaiwa kumchapa makofi mjamzito aliyejifungulia sakafuni.

Chama hicho kilikutana na kumhoji muuguzi huyo, Valentine Kinyaga, ambaye alikiri kutenda kosa hilo Januari 5, mwaka huu, majira ya saa nne usiku kwa kumpiga mama huyo makofi kutokana na kuingiwa na jazba, baada ya kujifungua sakafuni badala ya kuomba msaada kwake.

Makamu Rais wa TANNA, Ibrahim Mgoo, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kukutana na mama anayedai kufanyiwa kitendo hicho.

Mgoo alisema muuguzi huyo atapewa adhabu ili iwe fundisho kwa wauguzi wengine wenye tabia ya kuchafua taaluma hiyo kwa vitendo visivyo faa.

Pia, amewaonya wauguzi na wakunga nchini kuacha tabia ya kuwanyanyasa wagonjwa, hususani wajawazito. Alisema kwa yeyote akatayekamatwa akitekeleza kitendo hicho atapewa adhabu kali. Mgoo alibainisha kuwapo malalamiko mengi kutoka kwa wagonjwa hususani wajawazito, wakitendewa vitendo vya unyanyasaji na wauguzi, kitu ambacho ni makosa na ukiukwaji mkubwa wa maadili ya taaluma ya uuguzi.

Akizungumzia tukio la muuguzi kumzaba makofi mjamzito, Mgoo alisema siku ya tukio muuguzi huyo aliingia zamu ya usiku akiwa peke yake na kulikuwa na wajawazito 21 ambao aliwapa huduma wakati wanasubiri kujifungua. Usiku huo walijifungua wajawazito wanane na alikuwa na kazi nzito iliyomsababisha kuchoka.

"Kwakweli mtuhumiwa amekiri kutenda kosa la kumpiga makofi mwanamke huyo, lakini tunachomshukuru pamoja na kosa hilo alimhudumia mama huyo pamoja na mtoto wake aliyekuwa amekunywa maji mengi na kuokoa maisha ya mtoto huyo. Kwa sasa mama na mtoto wanaendelea vizuri," alisema Mgoo.

Alisema TANNA imebaini kituo hicho kuwa na upungufu mkubwa wa wauguzi, kwa kuwa uwiano ni muuguzi mmoja anapaswa kumhudumia mjamzito mmoja, lakini siku hiyo alihudumia wajawazito 21.

Kadhalika, aliiomba serikali kuajiri wauguzi wengine kwa kuwa ni miongoni mwa changamoto zinazojitokeza wakati wa kutoa huduma.



Mwonekano wa Ujenzi wa daraja la Mto Nkonjigwe katika kata ya Sasajila, wilayani Manyoni baada ya kukamilika ujenzi wake.
**PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# Kipanga aridhishwa usimamizi ujenzi chuo VETA

**Na Futuna Seleman**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, ameridhishwa na utendaji kazi wa kamati ya ujenzi inayosimamia mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi na Mafunzo ya Ufundi stadi (VETA), Korogwe ya mkoani Tanga.

Alisema hayo wakati akiwa katika ziara ya kukagua mradi huo ambao unasimamiwa na chuo cha VETA Kihonda cha mkoani Morogoro na kuridhishwa na hatua ya ujenzi iliyofikiwa pamoja na utaratibu mzima uliotumika katika kuutekeleza.

"Ndugu zangu kwa kweli mimi sina la kusema zaidi ya kuwapongeza sana kwa hatua ya ujenzi mliyofikia na nimeridhishwa na utaratibu mliotumia wa kupata mafundi jamii wanaotekeleza mradi huu," alisema Kipanga.

Kadhalika, aliwataka wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha vifaa vya upauaji vinapatikana mapema na kushauri matumizi ya jeshi la akiba kama vibarua ili ujenzi uweze kukamilika kwa muda uliopangwa.

"Kwa kuwa majengo karibu yote yamefikia hatua ya upauaji, nitoe rai kuwa vifaa vya upauaji vipatikane mapema ili ujenzi uendelee na kukamilika kwa wakati. Pia mnaweza kutumia jeshi la akiba kama vibarua kwa kuwa vijana hawa wapo wengi," alisema Kipanga. Naye Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Kissa Gwakisa, akiongea katika ziara hiyo, alisema wamefurahishwa na serikali kujenga chuo hicho katika wilaya yao na kuahidi kutoa ushirikiano ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa muda uliopangwa.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa chuo hicho, Mkuu wa chuo cha VETA Kihonda, Kashindye Maganga, alisema ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 34 na mpaka sasa wameshatumia Sh. milioni 918.




Mkuu wa Wilaya ya Urambo, Angelina Nkwingwa akipokea vifaa vya ujenzi, kutoka kwa Meneja wa benki ya NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, kwa ajili ya kumaliza ukarabati wa shule tatu zilizopo wilayani humo ikiwa ni mojawapo za jitihada za NMB kuunga mkono utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alilolitoa kwa mikoa yote nchini yenye upungufu wa vyumba vya madarasa. Kulia ni mbunge wa Urambo, Margaret Sitta. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANROADS yaagizwa kuendelea kuzoa mchanga Jangwani

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, anayeshughulikia sekta ya ujenzi, Elius Mwakalinga, amemuagiza Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa wa Dar es Salaam, Ngusa Julius, kuendelea na shughuli za utoaji mchanga katika Mto Msimbazi eneo la Jangwani, ili kudhibiti kero kipindi cha mvua.

Akizungumza mara baada ya kukagua na kuridhishwa na kazi inayoendelea katika eneo hilo, Mwakalinga alimuagiza Meneja huyo kuandaa mchoro utakaosaidia ufanisi wa kazi hiyo ili kutambua na kuyatafutia ufumbuzi maeneo yote yenye changamoto kubwa hasa kipindi cha mvua.

"Sisi kazi yetu si kupambana na maji, kazi yetu ni kuchimba eneo hili na kuelekeza maji sehemu ya kwenda, tunafanya hivi ili kupunguza athari za maji katika eneo hili," alisema Mwakalinga.

Pia, amemuagiza kufanya matengenezo mara kwa mara ili kuepusha serikali kutumia gharama kubwa ya matengenezo ya miundombinu linapotokea tatizo.

Kuhusu ujenzi wa daraja kubwa katika eneo hilo, Mwakalinga, alisema unaendelea vizuri na mchoro huo ukikamilika kazi hiyo itaanza mara moja.

Alisisitiza kwa sasa mpango wa serikali ni kukagua miundombinu yote ili kuhakikisha kunakuwa na usalama wakati wote.

Katika hatua nyingine, Mwakalinga, amekagua daraja la Pugu Kinyamwezi, Manispaa ya Ilala na kumtaka Meneja wa TANROADS mkoa wa Pwani kwa kushirikiana na uongozi wa Manispaa hiyo kupata ufumbuzi kuhusu kalvati la daraja hilo ambalo linatiririsha maji kwenye makazi ya watu.

Kwa upande wake, Meneja wa TANROADS mkoa wa Dar es salaam, Ngusa Julius, ameahidi kuyafanyia kazi maelekezo ya Katibu Mkuu na kusisitiza kuwa bado wanaendelea kusubiri ufumbuzi wa kudumu katika eneo hilo baada ya mchoro kukamilika.

"Hapa tunachokifanya kwa sasa ni kufanya matengenezo ya dharura ili kupunguza athari kwa wananchi na watumiaji wa barabara hii, wakati huo huo tukisubiri mwarobaini katika eneo hili," alisema

# Magereza yaokoa Bil. 11/- chakula cha wafungwa

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Magereza nchini limeokoa Sh. bilioni 11 za gharama ya chakula cha wafungwa tangu lianze kujitegemea ikiwa ni maelekezo ya Rais Dk. John Magufuli ya kulitaka jeshi hilo litumie nguvu kazi ya wafungwa kuzalisha.

Akizungumza juzi katika ziara ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, iliyofanyika katika Makao Makuu mapya ya jeshi hilo Msalato, jijini Dodoma, Kamishna Jenerali wa Magereza, Suleiman Mzee, amesema walikuwa wanatumia Shilingi bilioni moja kila mwezi kulipa wazabuni wa chakula waliokuwa wanauzia chakula jeshi hilo.

"Sasa hivi tunajitegemea asilimia kubwa kwa chakula, serikali kabla ya mwezi wa tatu, mwaka jana kila mwezi kulikuwa kuna deni la bilioni moja, lakini baada ya mwezi huo wa tatu sasa tunaokoa kiasi hicho cha fedha Shilingi bilioni moja na mpaka sasa tuna miezi kumi na moja tunajilisha wenyewe kupitia Shirika la Magereza," alisema CGP Mzee.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Naibu Waziri, Khamis Hamza Chilo, alilipongeza Jeshi la Magereza kwa kutekeleza vyema agizo la Rais Magufuli pamoja na ujenzi wa kiwanda kikubwa cha samani ambacho kikikamilika kitagharimu Sh. 1,101,743,123.

"Niwapongeze kwa hatua mbalimbali za maendeleo ambazo zingine nimeshuhudia mwenyewe, lakini kubwa kuweza kujitegemea kwa chakula cha wafungwa hali iliyookoa kiasi kikubwa cha fedha ambacho kinabaki humu humu ndani na mnakitumia kwa shughuli zingine za maendeleo hongereni sana," alisema Naibu

# Ataja vikwazo ukusanyaji taka

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya mji wa Kibaha, Mussa Ndomba, amesema vikwazo wanavyokumbana navyo katika usafi wa mji huo ni wananchi kushindwa kulipia kwa wakati fedha ya uzoaji taka.

Ndomba aliyabainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akiongea na waandishi wa habari kuwa baadhi ya maeneo wazabuni wanakwama kukusanya taka kutokana na kukosekana kwa fedha zinazotakiwa kuchangishwa na wananchi.

Alisema wananchi wanatakiwa kulipia fedha ya kukusanya taka kwa wakati ili wazabuni waendelee kuzikusanya kuanzia majumbani na maeneo ya biashara.

Ndoma alisema msisitizo unaendelea kutekelezwa na kamati za maendeleo za kata kwa kusimamia vizuri wazabuni lengo kuepuka magonjwa ya mlipuko katika mji huo.

" Suala la usafi kwa baadhi ya maeneo linakwamishwa na wananchi wenyewe kwa kushindwa kuchangia fedha za mzabuni wa kukusanya taka kwa wakati na hivyo kusababisha uchafu kuzagaa kwenye mazingira yao," alisema.

Alisema kwenye maeneo ambayo wananchi wanachanga fedha kwa kufuata utaratibu na mzabuni, akibainika kuwa kikwazo wanamtoa na kuweka mwingine.

Alisisitiza wananchi kuzingatia usafi wa mazingira kwenye maeneo yao ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko ambayo yanasababisha baadhi ya shughuli za uchumi na za kimaendeleo kusimama.

Mwenyekiti alisema katika kata zote 14 za halmashauri hiyo, zina wazabuni na endapo atakumbana na taka nyingi ambazo vifaa vyake havitoshelezi, halmashauri inatoa vifaa hivyo kwa gharama ya Sh. 50,000, lengo kusiwapo na eneo lenye uchafu unaozagaa na kuwa chanzo cha magonjwa.

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA PENALTI NYINGI MWAKA 2020 UK. 12-13




LAMPARD

# MAKOCHA WATANO WALIOKALIA KUTI KAVU MSIMU HUU

## ISIKUPITE

IKIWA ndiyo kwanza mwanzoni mwa mwaka, mshambuliaji wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo ndiye mchezaji mwenye wafuasi wengi zaidi kwenye mtandao wa Instagram baada ya kumaliza mwaka 2020 akiwa na wafuasi milioni 250 akifutiwa kwa mbali na Lionel Messi wa Baracelona na Argentina mwenye wafuasi milioni 174.



**LONDON,** England

MAKOCHA kadhaa wanaweza kupoteza kazi zao kwa kipindi ambacho hakitabiriki kwenye mchezo wa mpira wa miguu.

Mara zote timu inapofanya vibaya kuliko matarajio ya wengi, makocha ndio wanabeba mzio wa lawama.

Huku kukiwa kumebakiwa na nusu ya pili ya msimu huu wa ligi za soka Ulaya, makocha kadhaa kwenye klabu kubwa, wanaonekana ni kama wamekalia kuti kavu, kwani wanaweza kupoteza ajira yao wakati wowote.

Makala haya inawaangalia makocha watano ambao wanaweza kupoteza kazi zao kabla ya mwishoni mwa msimu huu...

### #5. RONALD KOEMAN (BARCELONA)

Ronald Koeman aliteuliwa kuwa kocha wa Barcelona kipindi cha majira ya joto mwaka 2020, huku klabu ikiwa na matarajio makubwa kutoka kwake.

Koeman amekumbana na mambo mengi pale Barcelona ndani ya uwanja na nje ya uwanjani. Hata hivyo, bado wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa LaLiga, wakipitwa pointi nne na vinara Atletico Madrid, wakiwa wamecheza mechi tatu zaidi ya kikosi hicho cha kocha Diego Simeone.

Hata kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Barcelona wapo kwenye droo ngumu hatua ya 16, wakikabiliana na Paris Saint-Germain kama ilivyokuwa msimu wa 2016-17.

Zaidi ni kwamba, kwa sasa Barcelona wapo kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu wa rais. Na mmoja wa wagombe amebainisha wazi kabisa kwamba kipaumbele chake cha kwanza akishinda ni kufumua benchi la ufundi, kitu ambacho kinaonekana wazi kwamba, ajira ya Koeman ipo shakani.

### #4. ANTONIO CONTE (INTER MILAN)

Antonio Conte ni kocha ambaye yupo kwenye presha kubwa baada ya kushindwa tena kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Inter Milan.

Katika kundi ambalo pia ilikuwapo Real Madrid, Shakhtar Donetsk na Borussia Moenchengladbach, Inter Milan ilimaliza nafasi ya nne. Hiyo maana yake ni kwamba, Nerazzurri hao hawatacheza Ulaya msimu huu.

Inter Milan kwa sasa wapo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Serie A, pointi tatu nyuma ya vinara AC Milan ambao ni wapinzani wao wa jiji moja.

Conte alikwaruzana na maofisa wa Inter kabla ya kuanza kwa msimu huu na ilionekana wazi kwamba angetupiwa virago. Hata hivyo, msimu huu kama atashindwa kubeba taji la Serie A kuna uwezekano mkubwa wa kupoteza kazi yake.

### #3. ANDREA PIRLO (JUVENTUS)

Wakati Andrea Pirlo alipoteuliwa kuwa kocha wa Juventus, mjadala mkubwa uliibuka. Bianconeri walimfukuza Maurizio Sarri licha ya kushinda taji la Scudetto.

Tofauti na matarajio yao baada ya kumfukuza Sarri, Juventus haijawa kwenye kiwango bora. Ingawa Juventus ina michezo miwili mkononi, wamepitwa pointi 10 na vinara wa Serie A, AC Milan.

Hata kama Juventus wakishindwa kutwaa taji la Serie A msimu huu, kama Pirlo atawaongoza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, anaweza kubaki klabuni hapo. Tofauti na hapo nafasi yake bado ipo shakani.

### #2. FRANK LAMPARD (CHELSEA)

Frank Lampard tayari yupo kwenye presha kubwa pale Chelsea. Blues hao wapo nafasi ya saba kwenye Ligi Kuu, wakiwa na pointi 29 kutokana na mechi 18.

Lampard amekuwa na asilimia mbaya zaidi ya kushinda kuliko kocha yeyote aliyepita pale Chelsea tangu zama za Roman Abramovich. Hivyo, licha ya kuwa gwiji wa klabu hiyo, uvumilivu unaweza kuwashinda wamiliki wake.

Msimu uliopita Chelsea ilitumia pauni milioni 250 kwa ajili ya kutengeneza kikosi kipya, lakini hadi sasa matokeo dimbani si ya kuridhisha. Kiungo huyo wa zamani wa Chelsea bado hajaweza kukitengeneza vizuri kikosi hicho licha ya usajili wa Timo Werner na Kai Havertz.

### #1. PEP GUARDIOLA (MANCHESTER CITY)

Pep Guardiola hajasaini mkataba mpya wa kuendelea kukaa pale Manchester City.

Hata hivyo, raia huyo wa Hispania nafasi yake inaweza kuwa shakani mwishoni mwa msimu huu. Msimu uliopita, City ilimaliza kwa kupitwa pointi 18 na Liverpool kwenye Ligi Kuu. Pia walipoteza kwa Lyon katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Msimu huu, pia wapo kwenye mbio za ubingwa. Lakini kiwango cha timu si cha kuridhisha sana. Hajawahi kuiongoza City zaidi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, bado hajawahi kushinda taji la Ligi ya Mabingwa katika kikosi alichokinoa kikiwa bila Lionel Messi.

Kama Manchester City watamaliza msimu huu bila taji lolote, ni wazi kwamba nafasi ya Pep Guardiola kuendelea na kazi yake ya ukocha pale kwenye dimba la Etihad itakuwa ngumu.

# WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA PENALTI NYINGI MWAKA 2020



BRUNO FERNANDES

**LONDON,** England

WAKATI soka lilitupa mambo mengi ya kuzungumza kwa mwaka 2020, moja ya topiki kubwa ambayo hatuwezi kuiacha ni VAR, athari yake na matokeo hasa kwa kutoa penalti.

**Kutokana na uiamuzi wake, VAR ilijadiliwa kwa kipindi cha mwaka mzima. Kulikuwa na nyakati timu zilibahatika na nyingine kulia.**

Julai 2020, Ligi Kuu Italia, Serie A, ilishuhudia msimu uliovunja rekodi kwa penalti nyingi.

Msimu wa 2018-19, jumla ya penalti 122 zilipatikana kwenye ligi hiyo. Lakini msimu uliofuata, idadi ilipaa hadi kufikia penalti 152 baada ya kila timu kufikisha mechi 30. Rekodi ya penalti nyingi 140 iliwekwa msimu wa 1949-50 kwenye Serie A.

Sawa na ligi nyingine, penalti nyingi zilitolewa kwa mwaka huo.

Makala haya inakuchambulia wachezaji waliofunga penalti nyingi zaidi katika ligi tano kubwa za Ulaya mwaka 2020.

### #10. ANDREJ KRAMARIC (1899 HOFFENHEIM/CROATIA) – PENALTI 7

Mchezaji wa 1899 Hoffenheim, Andrej Kramaric amecheza mechi 166 kwenye mashindano yote kwa klabu yake, lakini tayari ndiye mfungaji bora katika historia ya klabu hiyo, akiwa na mabao 83 kwa jina lake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alifunga mabao 25 katika mechi 36 kwa klabu.

Kwa mwaka 2020, raia huyo wa Croatia alifunga penalti saba, tano alifunga kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, moja kwenye Ligi ya Europa na moja kwenye Kombe la DFB-Pokal.

### #9. MOHAMED SALAH (LIVERPOOL/MISRI) – PENALTI 7

Mohamed Salah ameendelea kuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Liverpool kwa kiwango kisichoshuka. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amefunga mabao 111 katika mechi 177 kwa klabu hiyo.

Mwaka 2020 ulikuwa muhimu kwa Liverpool, ambapo kwa mara ya kwanza walitwaa taji la Ligi Kuu England kwa kipindi cha miaka 30. Salah alikuwa nguzo muhimu zaidi wakati Liverpool wakibeba taji hilo, huku akifunga penalti saba.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri, ameanza msimu wa 2020-21 kwa kasi kubwa, akifunga mabao 17 katika mechi 25, huku mabao sita yakiwa ya penalti.

### #8. NEYMAR (PARIS SAINT-GERMAIN/BRAZIL) – PENALTI 8

Neymar amefunga mabao mengi na penalti kwa kipindi chake cha uchezaji. Mambo hayajawa tofauti pale Paris Saint-Germain pia, nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, amefunga mabao 79 katika mechi 97 kwenye mashindano yote licha ya muda mwingi kukabiliwa na majeraha.

Katika mabao yake 320, alifunga kwa jina lake hadi sasa, 50 ameyafunga kwa penalti. Mwaka 2020, Neymar alifunga penalti nane - sita kwa PSG na mbili kwa Brazil.

### #7. LUCAS OCAMPOS (SEVILLA/ARGENTINA) – PENALTI 9

Lucas Ocampos alikamilisha uhamisho wa kwenda Sevilla, Julai mwaka 2019. Msimu wa 2019-20 ulimfanya yeye kufunga mabao 17 katika mechi 44 kwenye mashindano yote yakiwa mengi zaidi kwa msimu mmoja, huku matano kati yake yakiwa ni ya penalti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Argentina, amefunga mabao manne kwa msimu unaoendelea wa 2020-21, huku manne akifunga kwa penalti.

Kwa ujumla, Ocampos amefunga penalti tisa kwa mwaka 2020, na zote akiwa na klabu (nane kwenye LaLiga na moja kwenye mchezo UEFA Super dhidi ya Bayern Munich).

### #6. JORDAN VERETOUT (AS ROMA/UFARANSA) – PENALTI 9

Baada ya kucheza kwa mkopo kwa mwaka mmoja pale AS Roma, Jordan Veretout alijiunga kwa mkataba wa kudumu wa miaka minne na klabu hiyo Julai mwaka jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kwa sasa amecheza mechi 59 kwa klabu hiyo ya Serie A kwenye mashindano yote na kufunga mabao 15.

Mabao 11 kati ya hayo alifunga kwa penalti. Mwaka jana Veretout alifunga mabao 13, tisa kati yake kwa penalti.

### #5. LIONEL MESSI (BARCELONA/ARGENTINA) – PENALTI 9

Lionel Messi kwa sasa anaonekana kama anaelekea mwisho. Hata hivyo, mfungaji huyo wa wakati wote wa Barcelona bado ni mchezaji muhimu kwa timu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33, amefunga mabao 45 katika mechi 65 zilizopita kwa Barcelona, ametoa pasi za mwisho 33 kwa kipindi hicho.

Mwaka 2020, raia huyo wa Argentina alifunga penalti nane kwa Barcelona (tano kwenye LaLiga na tatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na moja kwa Argentina.

### #4. ROMELU LUKAKU (INTER MILAN/UBELGIJI) – PENALTI 10

Romelu Lukaku, ambaye amefunga penalti tatu msimu huu, anaonekana kama mchezaji muhimu zaidi kwa Inter Milan tangu alipotua hapo akitokea Manchester United. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amefunga mabao 50 katika mechi 71 tu kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo.

Kwa msimu huu 2020-21, Lukaku amefunga mabao 16 katika mechi 20 pekee kwa Inter, huku mabao matatu yakiwa ya penalti.

Alifunga penalti 10 mwaka 2020 - nane kwa Inter Milan na mbili kwa Ubelgiji.

### #3. CIRO IMMOBILE (LAZIO/ITALIA) – PENALTI 14

Tangu alipojiunga na Lazio Julai 2016, Ciro Immobile amekuwa mmoja wa mastraika wenye kiwango cha juu duniani.

Kwa sasa yupo katika msimu wake wa tano na klabu hiyo, na nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, amecheza mechi 196 kwenye mashindano yote na amefunga mabao 141.

Kwa kipindi chote cha kucheza soka, Immobile amefunga mabao 219 katika mechi 391, huku 55 kati yake ni kwa penalti. Mwaka 2020, mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia alifunga penalti 14 na zote kwa klabu.

### #2. BRUNO FERNANDES (MANCHESTER UNITED/URENO) – PENALTI 15

Bruno Fernandes alijiunga na Manchester United Januari 2020 kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 80. Katika miezi 12, amethibitisha kwamba ni usajili bora zaidi uliofanywa na klabu hiyo.

Katika mechi 47 alizowachezea 'Mashetani Wekundu' hao kwenye mashindano yote, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amehusika katika mabao 44, akifunga 27 na kutoa pasi za mwisho 17 na kwa sasa ni mchezaji muhimu kwa timu.

Mwaka 2020, alifunga penalti 15 kwa Manchester United (tisa kwenye Ligi Kuu, mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, tatu kwenye Ligi ya Europa na moja kwenye Kombe la FA).

### #1. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS/URENO) – PENALTI 17

Inawezekana kweli Cristiano Ronaldo asiwapo kwenye orodha hii? Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or yupo kwenye msimu wa tatu na klabu yake ya Juventus na tayari ameshaweka rekodi kadhaa.

Alimaliza msimu wa 2019-20 akiwa na mabao 37 kwenye mashindano yote katika mechi 46 mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi kwa msimu mmoja kwa Juventus.

Katika msimu huu unaoendelea, raia huyo wa Ureno tayari amefunga mabao 18 katika mechi 16 pekee.

Kwa sasa amefikisha mabao 758 kwa klabu na nchi yake. Ronaldo amefunga jumla ya penalti 133 kwa klabu na timu ya taifa.

Mwaka 2020, nahodha huyo wa Ureno alifunga penalti 17, zote kwa Juventus (13 kwenye Serie A, tatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na moja kwenye Coppa Italia).

## Nukuu

"Si kuhusu mimi. Nimekuja kwenye klabu ambayo inauhitaji sana. Kama nilibadilisha mawazo ya wachezaji wengine au mawazo yangu yalisaidia wachezaji wengine kuwa bora - labda. Lakini sidhani mimi nilibadilisha chochote kwa klabu kwa sababu kuichezea Manchester United kunamaanisha kucheza kwa shinikizo na uwajibikaji," **Bruno Fernandes kabla ya United kuivaa Liverpool kwenye mechi ya Ligi Kuu.**



"Acha nieleze. Fikiria nyuma yako wakati ulikuwa shuleni. Ni mwalimu gani unayemkumbuka zaidi? Si yule aliyekurahisishia maisha na hakutarajia chochote kutoka kwako, hapana, hapana, hapana. Unakumbuka mwalimu mbaya, yule ambaye alikuwa mkali kwako. Yule aliyekupa shinikizo na alifanya kila kitu ili kupata kitu bora kutoka kwako. Huyo ndiye mwalimu aliyekufanya uwe bora, sivyo? Na Jurgen Klopp alikuwa hivyo kwangu wakati," **Robert Lewandowski akizungumzia namna Klopp alivyomfanya kuwa bora wakati wakiwa Borussia Dortmund.**



"Dhamira yetu ni moja kwamba, tunataka ushindi kwenye kila mchezo na tunataka kuchukua taji msimu huu, na hilo naliona linakuja kwa sababu wachezaji wanaonyesha moyo wa kupambana na hawaonyeshi kuchoka katika hilo," **Kocha wa Manchester United, Ole Gunner Solskjaer, baada ya United kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Burnley wiki iliyopita.**



# DIRISHA DOGO LILIVYOMIMINA MAPRO LIGI TANZANIA BARA

Na Adam Fungamwango

INAONEKANA kabisa kuwa bado Tanzania inahitaji baadhi ya wachezaji wa kigeni kwa ajili ya kulichangamsha soka la na kuwafanya wachezaji wazawa kujituma.

**Kwenye dirisha dogo la usajili lililomalizika Januari 15, mwaka huu kwa namna ambayo haikutarajiwa, klabu nyingi zimeongeza wachezaji mbalimbali, wakiwamo wa kigeni.**

Kilichoshangaza zaidi ni kwamba kwenye dirisha hili, hata klabu ambazo ni nadra sana kusajili wachezaji wa kigeni zimefanya hivyo. Ni kwamba baadhi ya makocha wanaozifundisha timu mbalimbali wameona kuwa matatizo makubwa kwa wachezaji wa Kitanzania ni safu ya ushambuliaji.

Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, alikaririwa hivi karibuni kuwa ameangalia Ligi Kuu ya Tanzania, alichobaini ni kwamba kuna tatizo kubwa kwenye ufungaji hasa kwa wachezaji wa Kitanzania na ndiyo maana timu zinafungana mabao machache.

Akasema idadi ya matokeo mengi yanakuwa ni 1-0 au 2-1 na kama idadi ya mabao inakuwa kubwa basi ni kwa zile timu ambazo zina wachezaji au washambuliaji wa kigeni. Pamoja na hayo, tumeona kuna timu zimesajili makipa, mabeki, viungo wa kukaba na viungo washambuliaji na mastraika.

Kwenye makala haya tunawaangalia baadhi ya wachezaji wa kigeni waliosajiliwa na klabu mbalimbali za Ligi Kuu kipindi cha dirisha hili dogo...



Straika mpya wa Simba, Perfect Chikwende, akitia saini mkataba wa miaka miwili wa kujiunga na timu hiyo katika dirisha dogo lililofungwa Januari 15, mwaka huu. **PICHA: SIMBA**

**#1. MATHIAS KIGONYA - AZAM (KIPA)**

Ni golikipa raia wa Uganda ambaye alikuwa akiichezea Forest Rangers ya Zambia. Azam FC imemsajili kipa huyo kwa mkataba wa miaka miwili, baada ya makipa wao Watanzania David Kissu na mwenzake Benjamin Haule, kuonekana wana makosa mengi yaliyosababisha kupoteza pointi nyingi kwenye kinyang'anyiro cha kuwania ubingwa wa Tanzania Bara mbele ya Simba na Yanga.

**#2. LUTIMBA YAYO - MBEYA CITY (BEKI)**

Katika hali isiyotarajiwa, timu ya Mbeya City imesajili mchezaji wa kigeni kutoka Uganda. Anaitwa Yayo Lutimba, mtoto wa straika hatari wa zamani wa Uganda, Lutimba Yayo. Huyu anachezea beki wa kushoto. Inaonekana ni kwa matakwa ya kocha Lule ambaye pia ni Mganda. Kwa kawaida timu kama Mbeya City ni nadra sana kuwa na wachezaji wa kigeni.

**#3. PASCHAL KITENGE - COASTAL UNION (BEKI)**

Coastal Union safari hii nayo imekwenda nchini DR Congo na kuleta kifaa. Ni beki wa kati, Paschal Kitenge akitokea AS Nyuki ya Congo DR. Amesaini mkataba wa mwaka mmoja na nusu kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo kusaidia safu ya ulinzi ya kikosi hicho.

**#4. TOUYA JEAN DIDIER - MBEYA CITY (KIUNGO)**

Huyu ni kiungo mshambuliaji raia wa Burundi. Amesajiliwa na Mbeya City ambayo inaonekana kujidhatiti ili kubaki Ligi Kuu. Kabla ya kujiunga na timu hiyo, alikuwa akiichezea klabu ya Musanse ya nchini Burundi.

**#5. TADDEO LWANGA - SIMBA (KIUNGO)**

Simba imemsajili Mganda Taddeo Lwanga kwa ajili ya kuziba pengo la kiungo mkabaji, baada ya Mbrazil Gerson Fraga kuumia na kuondolewa kwenye orodha ya wachezaji wa kigeni. Lwanga, ambaye ni mchezaji wa timu ya Taifa ya Uganda, alianza kuonekana kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi mjini Zanzibar.

**#6. FRANCIS MUSTAPHA - COASTAL UNION (KIUNGO)**

Ni mchezaji kutoka nchini Burundi ambaye amesaini mkataba wa mwaka mmoja kuichezea Coastal Union. Kiungo huyo mshambuliaji mwenye uwezo mkubwa wa kufunga mabao, amesajiliwa akitokea klabu ya Buserega ya nchini Rwanda, akiwa amezichezea klabu ya Gor Mahia ya Kenya na Kiyovu Sport ya Rwanda.

**#7. SAIDO NTIBAZONKIZA - YANGA (STRAIKA)**

Nadhani huyu ndiye mchezaji anayeshikilia rekodi ya kuwa wa kwanza kusajiliwa kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo. Mkataba wake na Yanga ulikuwa kabla hata dirisha kufunguliwa. Lilipofunguliwa tu, akakamilisha taratibu na akaanza kucheza, kabla klabu nyingi kufanya usajiliwa wa dirisha dogo.

**#8. MPIANA MONZINZI - AZAM (STRAIKA)**

Azam imeamua kusajili straika baada ya kuachana na baadhi ya wachezaji wake ambao hawakukidhi mahitaji, huku Prince Dube akiwa majeruhi. Mpiana Monzinzi ambaye ni raia wa DR Congo, amesaini kwenye klabu hiyo akitarajiwa kuongeza nguvu safu ya ushambuliaji ambayo baada ya majeraha ya Dube, imekuwa ikisuasua.

**#9. FISTON ABDULRAZACK - YANGA (STRAIKA)**

Kwenye dakika za mwisho za usajili wa dirisha dogo, Yanga imeshusha kifaa kiitwacho Fiston Abdulrazack. Ni straika raia wa Burundi ambaye Yanga imemsajili kutokana na kuwa na matatizo kwenye safu yake ya ushambuliaji. Straika huyo mara ya mwisho alikuwa akiichezea klabu ya ENPPI ya nchini Misri.

**#10. PERFECT CHIKWENDE - SIMBA (STRAIKA)**

Moja kati ya usajili wa dakika za mwisho kwa klabu ya Simba ni wa Perfect Chikwende raia wa Zimbabwe. Kwa siku za karibuni alijizolea umaarufu baada ya kuifunga Simba kwenye mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika akiwa na timu ya FC Patinum. Ingawa hakufunga kwenye mechi ya marudiano, lakini bado alionekana kuwa mchezaji msumbufu, kiasi cha klabu nyingi Tanzania kumhitaji. Na kweli, ameibukia Simba ambayo itamtumia kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika.

**JE, WAJUA?**



WAKATI wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Southampton, Jamie Vardy, alipiga mashuti saba bila kufunga, idadi ambayo ni kubwa zaidi kwake kufanya hivyo pasipo kufumania nyavu kwenye Ligi Kuu England, lakini pia amekutana na timu hiyo mara saba nyumbani kwenye Uwanja wa King Power bila kuzifumania nyavu katika ligi hiyo.

## HABARI DODOMA



# Bilioni 28/- kusambaza umeme maeneo mapya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) Mkoa wa Dodoma, linatarajia kutumia Sh. bilioni 27.7 kusambaza umeme kuyafikia maeneo mapya yanayokua kwa kasi ndani ya Jiji la Dodoma.

Meneja wa shirika hilo mkoani hapa, Frank Chambua, aliyasema hayo jana katika kikao kilichowakutanisha wakuu wa taasisi za kiserikali za jiji hilo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alikuwa akipokea taarifa ya mipango ya upelekaji huduma kwenye maeneo ya uwekezaji na yanayojengwa kwa kasi jijini hapa.

Alisema shirika limejipanga kujenga miradi hiyo mipya ya kuunganisha wateja kwenye maeneo yanayokua kwa kasi.

Meneja huyo alisema mipango ya muda mfupi ya shirika ni kujenga miradi mipya ya kimkakati itakayogharimu Sh. bilioni 3.3 ikiwamo eneo la viwanda la Nala.

"Katika ziara yetu tuliyofanya na Mkuu wa Mkoa mwishoni mwa mwaka jana, kuna baadhi ya maeneo tulipita na yakaainishwa ili yatengenezewe mkakati wa kupeleka umeme kwenye maeneo hayo, mojawapo ni Nala.

"Tumefanya tathmini na kubaini kwamba kupeleka umeme pale zinahitajika Sh. milioni 678, mradi bado haujaanza tupo kwenye harakati za kutafuta fedha," alisema.

Alisema katika eneo la viwanda Nala zinahitajika Sh. bilioni 1.5, Mahungu Sh. milioni 695 na eneo la Iyumbu jirani na shule ya mfano zinahitajika Sh. milioni 188.

"Eneo lingine ni Michese ambako zinahitajika Sh. milioni 168, tumepata Sh. milioni 25, eneo la Mkalama zinahitajika Sh. milioni 84 na tayari tumepata Sh. milioni 11 mradi unaendelea.

"Upanuzi wa kituo cha Zuzu umekamilika, umegharimu Dola za Marekani milioni 53, kuna mpango wa ujenzi wa njia nane za umeme za msongo wa kilovolti 33 kupeleka maeneo tofauti zenye jumla ya urefu wa kilomita 153.9 zinazokadiriwa kugharimu Sh. bilioni 9.3," alisema.

Meneja huyo alisema kwa sasa kuna kiasi kikubwa cha umeme cha Megawati 248 kwa Jiji la Dodoma na kituo kingine cha Kondoa-Bicha kina Megawati 13.4, wakati matumizi ya juu kwa jiji hilo ni Megawati 36 na Kondoa matumizi ni Megawati tano, hivyo kuna ziada ya Megawati 221.4.

Akizungumzia makadirio ya mahitaji ya umeme kwa jiji hilo miaka 20 ijayo, meneja huyo alisema kutakuwa na mahitaji ya Megawati 250 ifikapo mwaka 2040 kutokana taarifa za mipango ya uwekezaji jijini hapa.

Katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Mahenge, alishauri kuainishwa maeneo machache ya kipaumbele hasa ya uwekezaji kama vile Nala, ili kupeleka huduma ya umeme na kuvutia wawekezaji, huku Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, akisema hadi sasa kuna wawekezaji 15 wa uhakika wamejitokeza kutaka kuwekeza Dodoma.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mbunge wa Jimbo la Chamwino, Deogratius Ndejembi, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mditi Wilaya ya Chamwino Mkoani Dodoma mwisho wa wiki alipofika hapo kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya watoto wa kidato cha kwanza, Mbunge huyo alichangia mifuko 430 ya saruji na Sh. milioni 15 kwa ajili ya ujenzi huo kwa baadhi ya shule za Kata za Itiso, Zajilwa na Haneti za wilaya hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC: Pandeni miti kukabili mabadiliko ya tabianchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewahimiza Watanzania kulinda mazingira yanayowazunguka kwa kupanda miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Amesema kila Jumamosi asubuhi mkoani humo ni siku ya kupanda miti kwenye maeneo ya wazi isipokuwa Jumamosi ya mwisho wa mwezi ambayo ni siku ya usafi.

Akizungumza juzi baada ya kupanda miti katika eneo ya wazi la Iseni Park jijini hapa, Dk. Mahenge alisema kila Mtanzania anapaswa kuhamasika katika kulinda mazingira na kujenga utamaduni wa kupanda miti.

"Ni wajibu kwa kila Mtanzania kuona umuhimu wa kupanda miti katika maeneo kwa kuwa ni urithi pekee tulioachiwa katika sayari hii, tangu sayari hii iumbwe haiongezeki wala kupungua ndiyo tunayoishi na rasilimali tulizoachiwa zinazidi kupungua, mito mingi inakauka, ni wajibu wetu kuendelea kulinda," alisema.

Dk. Mahenge alisema maendeleo ya teknolojia duniani yameathiri uoto wa asili na ili kuurudisha, ni lazima kutunza mazingira na kuendelea kupanda miti katika maeneo yaliyowazi.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema eneo hilo lililopandwa lina ekari 37 kwa ajili ya kupumzikia kutokana na baadhi ya maeneo yanayolizunguka eneo hilo kujengwa taasisi za kiserikali.

"Leo (juzi) imepandwa miche 3,700 na ni zoezi endelevu katika maeneo yote, tunahimiza watendaji wa kata kusimamia zoezi hili katika maeneo yao kuhakikisha linafanikiwa," alisema.

Meneja wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Kati, Mathew Kiondo, alizitaka taasisi na wananchi kuhakikisha miti inayopandwa katika maeneo mbalimbali, wanaitunza baada ya mvua kuisha ili istawi.

Alisema TFS watatoa ushirikiano katika kutoa wataalamu na miti inayopandwa na kuisimamia na kuhimiza wananchi kupanda kwa wingi.

"Sisi TFS tutaweka matenki ya maji kama tulivyofanya Medeli na hapa tutaweka matenki ya maji kusaidia kipindi mvua zikiacha kunyesha, miti iendelee kutunzwa," alisema.

# TARI yawapa mbinu wakulima wa zabibu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Kituo cha Makutupora, imewataka wakulima wa zabibu kuzingatia ushauri wa watafiti, ili kuongeza thamani ya zao hilo.

Mtafiti katika kitengo cha uchumi wa jamii wa kituo hicho, Devotha Mchau, alitoa rai hiyo jana alipozungumzia uongezaji thamani zao hilo katika ziara ya waandishi wa habari na watafiti waliotembelea kituo hicho.

Alisema zabibu hupandwa kwa misimu miwili, hivyo wakulima ni muhimu kuzingatia ushauri wa watafiti na kupata elimu ya utengenezaji mvinyo ili kujiongezea kipato.

"Unakuta wakulima wengi wanaendesha kilimo hicho bila kuwa na elimu ya kuongeza thamani zao hilo, ndiyo maana ninasisitiza wajitokeze katika vituo vya utafiti kupata mafunzo hayo," alisema Mchau.

Alisema wakulima wakipata elimu hiyo na kufuata taratibu za upandaji mpaka uvunaji, itasaidia kuvuna kwa wingi na kupata faida kubwa.

Mtafiti huyo aliwataka wakulima kufuata kanuni za utunzaji wa zao hilo ili kupata mavuno mengi.

"Zao la zabibu linahitaji sana uangalizi wakati wa kupanda mpaka mavuno, wakulima mkizingatia hayo, mtazidi kukua kiuchumi kupitia zao hilo," alisema Mchau.

Mtafiti mwingine wa kituo hicho, Stellah Hangambagi, alisema hali ya hewa ya Dodoma inaruhusu kulima zao hilo, hivyo wakulima wanapaswa kuchangamkia fursa hiyo iwainue kiuchumi.

"Zao la zabibu linapendwa duniani kote na Dodoma imebarikiwa kuwa sehemu ambayo zao hilo linastawi, wakulima tumieni nafasi hii kujikwamua kiuchumi," alisema Hangambagi.

Alishukuru serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ambayo imekuwa ikitoa fedha kwa vituo vya utafiti wa kilimo.





# Shule za sekondari Wazazi kubadilishwa matumizi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya shule za sekondari zinazomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), katika Mkoa wa Mbeya zitabadilishiwa matumizi baada ya kushindwa kujiendesha na kulimbikiza madeni ya kila mwaka, Sh.bilioni moja.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Taifa, Dk. Edmund Mndolwa, wakati wa kikao kilichowahusisha wakuu wa shule, bodi na wenyeviti wa Jumuiya hiyo katika wilaya zote za Mkoa wa Mbeya.

Dk. Mndolwa alisema mpango uliopo ni kubakisha shule tano kati ya 14 zinazomilikiwa na Jumuiya hiyo mkoani Mbeya na kwamba zitakazobaki zitafaulisha wanafunzi na kupangiwa matumizi mengine.

Aliitaja moja ya shule itakayobadilishiwa matumizi ni pamoja na shule kongwe ya Sekondari ya Meta ambayo itakuwa ya mchepuo wa Kiingereza.

Alisema shule hiyo pamoja na Chunya Sekondari, zimeshindwa kujiendesha kutokana na kuwa na madeni mengi ikiwamo mishahara ya walimu ambao wanadai kwa kipindi kirefu.

"Shule hizi zimekuwa zikijiendesha kwa hasara kubwa hakuna faida tunayoipata, hadhi ya shule kwa sasa ni tofauti na zamani, tunahitaji kubadili mfumo wa uendeshaji kuanzia kwa wakuu wa shule, walimu na bodi, haiwezekani Sekondari ya Meta ikiwa na mwanafunzi mmoja tu wa kidato cha kwanza hii ni aibu," alisema Dk. Mndolwa.

Alisema katika kipindi cha utawala wake hatakubali kuona shule hizo zinakufa na tayari ameandaa mpango wa namna shule zote nchini zitaendeshwa ikiwa ni pamoja na baadhi kutoa huduma nyingine ili zilete faida kwa Jumuiya.

Aliwaasa wakuu wote wa shule za sekondari zinazomilikiwa na jumuiya hiyo kuzingatia maelekezo ya kutumia mfumo wa akaunti ya pamoja kwa shule zote nchini (Control Account) ili kujua mapato na matumizi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasoke, alibariki wazo la shule zilizoshindwa kujiendesha kubadili matumizi na kutoa huduma nyingine za kijamii ili Jumuiya hiyo iendelea kupata faida.

Alisema kwa sasa Jumuiya ina mzigo mkubwa wa madeni ambao umechangiwa na usimamizi mbovu wa shule hizo na badala yake wachache kujinufaisha.

Mwanasheria wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, Wakili Beatus Mafuru, alisema ana orodha ya shule zote pamoja na walimu na wenyeviti wa bodi ambao wamehujumu shule hizo na kuzisababishia hasara.

Alisema waliohusika watafunguliwa kesi ya jinai pamoja na kulipa fedha zote walizozitumia kinyume na taratibu za uendeshaji wa shule hizo na kusisitiza kuwa zitumie mfumo wa 'Control Account' ili kuondoka makandokando.

Katibu Mwenezi na Itikadi CCM mkoa, Bashiru Madodi alisema moja ya sababu shule hizo kushindwa kujiendesha na kuwa na deni kubwa ni baadhi ya viongozi wa juu kula sahani moja na wakuu wa shule.

Alisema ili kuondoka tatizo hilo viongozi wa juu wanapaswa kusimamia kikamilifu uendeshwaji wa shule hizo ili kuziba mianya ya matumizi mabaya ya fedha ikiwa ni pamoja na kugawana mishahara kinyemela.



Mbunge wa Jimbo la Mbeya mjini (aliyevaa miwani). Dk. Tulia Akson, akipewa mkono wa ahsante na baadhi ya viongozi wa Shule ya Sekondari ya Pankumbi ambapo alichangia mifuko 100 ya Saruji kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa mwishoni mwa wiki.**PICHA GRACE MWAKALINGA**

## Dk. Tulia achangia mil. 8/- ujenzi msikiti

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya, Dk. Tulia Ackson, amechangia Sh. milioni nane katika harambee ya ujenzi wa Msikiti wa Alqaadiriya uliopo Kata ya Itezi.

Alitoa msaada huo mwishoni mwa wiki katika harambee hiyo aliyokuwa mgeni rasmi na kwamba kiasi hicho cha fedha kitaweza kununua nondo, saruji, mbao, mchanga na kokoto.

Katika harambee hiyo Dk. Tulia aliwaasa waumini wa dini ya Kiislam kuendelea kushikamana na kuwa kitu kimoja katika kuyaenzi maagizo ya Mungu.

Alisema waumini wakiendelea na mshikamano huo basi ujenzi wa msikiti huo utakamilika haraka na kuanza kutoa huduma, lakini kukiwapo na migogoro watakwamisha jitihada zao.

"Katika kuunga mkono jitihada mlizozifanya, tumekuja na baadhi ya mahitaji ambayo ni pamoja na saruji, nondo, misumari, mbao, mchanga, kokoto vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni nane na nawaahidi kwamba huu sio mwisho ntaendelea kutoa mchango wangu kadri hatua za ujenzi zinapofikia alisema Dk. Tulia.

Aliwaomba wadau na waumini wengine wa dini hiyo ndani na nje ya nchi kusaidia ujenzi huo ambao unahitaji mamilioni ya fedha kukamilika.

Diwani wa Kata ya Itezi, Sambwe Shitambala, alipongeza hatua ya waumini wa msikiti huo kutoa nguvu kazi na mali zao kwa ajili ha ujenzi wa msikiti mpya na kwamba ataendea kuhamasisha viongozi wengine kuchangia.

Katika hatua nyingine, Dk. Tulia alitoa msaada wa mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Pankumbi.

# Kudorora bei ya mchele kwaathiri wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

KUDORORA kwa bei ya bidhaa ya mchele kumeleta athari kwa baadhi ya wakulima wilayani Mbarali na kusababisha kukosa fedha za kuandaa mashamba ya mpunga msimu huu wa kilimo.

Wakizungumza juzi na wilayani humo, baadhi ya wakulima walisema miaka ya nyuma msimu kama huu mchele huuzwa kati ya Sh. 1,800 hadi 2,000 kwa kilo moja, lakini kwa sasa bei yasokoni ni kati ya Sh. 1100 na 1,500. Wille Mwakasoke, mkulima kutoka Igurusi wilayani humo ambaye pia ni mjasiriamali, alisema gharama za uzalishaji wa zao hilo ni kubwa ikilinganishwa na bei ya soko, hali inayowapa wakati mgumu wakulima kumudu gharama hizo. Alisema kuyumba kwa bei ya mchele kuna athiri baadhi ya shughuli nyingine za kiuchumi zikiwamo biashara ndogo ambazo hutegemea mzunguko wa fedha unaotokana na biashara hiyo.

"Mwezi kama huu na kuendelea wakulima huwa wanauza kilo 20 za mchele kati ya Sh. 36,000 na 40,000, tofauti na mwaka huu ambapo bei iko chini sana na soko liliyumba tangu mwaka jana wakati changamoto za kipindi cha corona," alisema Mwakasoke.

Huruma Mwakanyamale, muuza nafaka ikiwamo mchele, alisema licha ya bidhaa hiyo kuuzwa kwa bei ya chini, lakini hata kasi ya utokaji ni ndogo ikilinganishwa na kipindi cha nyuma kabla ya janga la corona.

"Ingawa tumeanza kujijenga upya kibiashara baada ya kipindi cha mpito cha corona kati ya mwezi Machi na Mei 2020, jitihada zetu hazifikiwi haraka kutokana ukosefu wa soko la uhakika hasa kwa mchele ambao ni zao kuu kwa Wilaya ya Mbarali," alisema Mwakanyamale.

Emmanuel Mtaki, miongoni mwa vijana ambao mwaka huu hawezi kujihusisha na shughuli za kilimo baada ya kukosa mtaji, alisema kuwa pamoja na familia yake wameamua kujaribu shughuli ya kuuza chips ili kuendesha maisha yao.

"Mimi ni mkulima, lakini kwa msimu huu nimekwama kuendeleza shughuli hiyo, kutokea kwa janga corona mwaka jana kuliyumbisha mtaji wangu, sitakuwa na uwezo wa kumudu gharama za kilimo hasa kama kukodi shamba, kununua pembejeo na uwezo wa kupata rasilimali watu" alisema Mtaki.

Hivi karibuni Ofisa Biashara Mkoa wa Mbeya, Stanley Kibakaya, alisema kuwa kushuka kwa bei ya bidhaa kama mchele na mahindi inatokana na uzalishaji wa mazao hayo kuwa mengi.

Alisema moja ya mambo wanayotakiwa kuyafanya wakulima ni kutunza baadhi ya mazao yao ghalani wakisubiri bei kupanda baada ya msimu wa kilimo kumaliza na kuendelea kuongeza thamani ya mazao hayo kuwa bidhaa mfano kutengeneza unga wa lishe ili wasipate hasara.



## HABARI ZANZIBAR

# Moto ulioteketeza hoteli mbili wazimwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KIKOSI cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kwa kushirikiana na viongozi, wafanyakazi wa hoteli na wananchi wa maeneo jirani wamefanikiwa kuuzima moto mkubwa uliozuka usiku wa manane na kuteketeza baadhi ya majengo ya hoteli za Ocean Paradise na Tui Blue Bahari zilizopo pwani Mchangani, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Askari wa kikosi hicho kutoka vituo vya Mahonda na Kigunda, walifika eneo hilo ndani ya muda wa dakika 18 baada ya kuibuka tukio hilo lililoripotiwa kuanza kutokea majira ya saa 8.33 za usiku, juzi.

Harakati za kuuzima moto huo zilianza mara moja zikishirikisha pia wafanyakazi wa hoteli jirani zinazozunguka hoteli hizo mbili na kufanikiwa kukamilika uzimaji majira ya saa tatu asubuhi kwa kupata nguvu za ziada kutoka makao makuu ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Kilimani, mjini Zanzibar.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akiambatana na viongozi tofauti wa sekta ya utalii walifika eneo la tukio kujionea hali halisi ya hasara iliyotokana na janga hilo pamoja na kuwapa pole viongozi na wafanyakazi wa Ocean Paradise na Tui Blue Bahari kwa vile ni wadau wakubwa katika kuchangia Pato la Taifa.

Akitoa taarifa za awali kuhusu tukio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema wageni wote waliokuwamo kwenye hoteli hizo mbili wako salama wakati moto huo ulipoanza kuibuka katika jengo la ufundi la hoteli ya Ocean Paradise.

Ayoub alisema kasi ya moto huo ilianza kuenea katika tangi la mafuta, mgahawa ndani ya hoteli ya paradise na baadaye kusambaa katika hoteli ya Tui Blue Bahari uliathiri sehemu ya mapokezi, utawala pamoja na vyumba vya kulala wageni vipatavyo 96.

Naye Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Leila Mohamed Mussa, alisema wageni 208 wa Hoteli ya Ocean Paradise yenye Wafanyakazi 170 na wageni 129 wa Hoteli ya Tui Blue Bahari yenye wafanyakazi 300 wazawa, wamehamishiwa hoteli za jirani.

Leila Mohamed alimueleza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwamba hatua hiyo ya hifadhi ya wageni hao inatokana na utaratibu wa maombi mapya ya wageni wanaotaka kuitembelea Zanzibar kipindi hiki.

Waziri huyo wa Utalii na Mambo ya Kale aliwapongeza viongozi na wafanyakazi wa taasisi zinazosimamia kutembeza watalii nchini kwa kazi kubwa waliyoifanya kusimamia uzimaji moto licha ya changamoto ya baadhi ya wageni kuamua kuendelea kubakia katika maeneo hayo. Hemed aliwahakikishia wawekezaji wa sekta ya utalii nchini kwamba Serikali Kuu itaendelea kutoa ushirikiano wa kina kuona uhalisia wa majengo ya hoteli hizo mbili yanarejea na kuanza kutoa huduma kama kawaida.

Aliipongeza Taasisi ya Bima ya Jubilee kwa uharaka wale iliyoonyesha ya wataalamu wake kuanza tathmini ya hasara iliyotokea katika Hoteli ya Tui Blue Bahari ili walipe bima katika kipindi kati ya mwezi mmoja na miwili baada ya ripoti husika.

Alimuagiza Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuifuatilia taasisi ya bima inayohudumia Hoteli ya Ocean Paradise kuanza tathmini mara moja baada ya tukio hilo ili kuwarejeshea imani wateja wao.

Alisema uwapo wa hoteli hizo mbili zinazolipa kodi kwa zaidi ya Sh. bilioni mbili kila moja kwa mwaka, lazima uthaminiwe kwa vile unachangia mapato ya taifa yanayoendelea kutumiwa katika huduma mbalimbali za kijamii na miundombinu tofauti ya serikali.

Wakielezea faraja walioipata kutokana na ujio wa viongozi hao wa serikali ikiwa ni njia ya kuwapa pole, Meneja Mkuu wa Hoteli ya Tui Blue Bahari, Reda Sweed na wa Hoteli ya Ocean Paradise, Burnt walisema ushirikiano wa pamoja uliofanikisha kukabiliana na janga hilo wataendelea kuukumbuka katika maisha yao ya baadaye.

# Sheria yaruhusu watatu kuingiza vileo Z'bar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema watu wanaoruhusiwa kuingiza vileo (pombe) visiwani humo ni watatu pekee kwa mujibu wa sheria mpya ya udhibiti na ushauri wa usimamizi wa vileo namba 9 ya mwaka 2020.

Hayo yameleezwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum, Masoud Ali Mohammed alipokuwa akizungumza katika mkutano wa waandishi wa habari ofisini kwake Vuga, kuhusu utekelezaji wa sheria ya mpya ya vileo.

Alisema kuwa kabla ya sheria hiyo kupitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar (BLW) na kusainiwa na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein mwaka 2020, pia ilijadiliwa na makatibu wakuu pamoja na wadau katika sekta ya vileo visiwani humo.

Waziri Masoud alisema lengo la kutungwa sheria ya vileo Zanzibar ni kuweka udhibiti wa uingizaji na usababazaji wa pombe pamoja na kuondoa malalamiko kutoka kwa wananchi biashara hiyo kufanyika karibu na maeneo ya huduma za jamii zikiwamo nyumba za ibada, shule hospitali vituo vya daladala na vyuo vya madrasa.

"Kimsingi mimi nasimama katika sheria na imeleeza watu au kampuni zinazotakiwa kuingiza vileo ni tatu Zanzibar huo ndio msimamo wa sheria, lakini kama kumejitokeza changamoto za utekelezi wa sheria kuna taratibu zake za kutafuta ufumbuzi bila ya kuvunja sheria....," alisema Waziri Masoud.

"Huwezi kuelekeza nje ya sheria, waziri anachoweza kusema sheria zizingatiwe na busara itumike, lakini waziri huwezi kuelekeza nje ya sheria maana yake utakuwa sehemu ya kuvunja sheria wakati jukumu lako ni kulinda sheria..."

Alisema sheria hiyo imetungwa kwa madhumuni ya kudhibiti na kuweka utaratibu mzuri wa kisheria katika biashara ya vileo na kwamba ni muhimu bodi ikaendelea kutoa elimu ili wadau wa biashara hiyo na wananchi wapate kuifahamu sheria mpya.

"Changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa sheria mpya ya vileo usiwe mwanya wa kuvunja sheria, malengo makubwa ya kutungwa sheria hii yalikuwa kuweka utaratibu mzuri wa kisheria wa uingizaji vileo na usambazaji," alisema Waziri Masoud.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Udhibiti na Ushauri wa Vileo Zanzibar, Abdulrazaki Abdulkadiri Ali, alisema wameamua kutoa vibali vya uingizaji vileo kwa kampuni sita badala ya tatu licha ya kuwa kinyume na sheria kwa kutumia hekima na busara ili kulinda mapato ya serikali kupitia kodi za vileo.

Alisema uamuzi huo umefikiwa baada ya kufanyika vikao vya pamoja kati ya wadau wa vileo, waziri mwenye dhamana pamoja kikao cha viongozi wawili waandamizi wa Ikulu kabla ya kuweka sheria kando.

"Baada ya kushauriana katika Kikao cha pamoja kati ya waziri na wadau wa vileo kabla ya bodi kukutana na viongozi waandamizi wa Ikulu, Hasinuu Makame na Suleiman Haji, tumeamua kutoa vibali kwa kampuni sita badala ya tatu ili kulinda mapato ya serikali," alisema.



Watalii kutoka Poland (pichani), wakipata historia ya mti ujulikanao kama Mbula ulioko nyuma ya Ngome Kongwe Mjini Unguja, kama walivyokutwa na mpiga picha, jana. **PICHA: MARTINE KAMBEMBA**

# Ziara za viongozi zasaidia uteketezaji bidhaa mbovu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

ZIARA za viongozi wa kitaifa za mara kwa mara katika Bandari ya Malindi zimesaidia wafanyabiashara kuwa tayari kugharamika kuteketeza bidhaa zao zinapoharibika bila ya kuweka vikwazo.

Mkurugenzi Idara ya Udhibiti Usalama wa Chakula na Dawa wa Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA), Dk. Khamis Ali Omar, alisema hayo mbele ya waandishi wa habari jana katika dampo la Kibele wakati wa kuangamiza tani 15 za unga wa ngano ulioharibika ambao uliongizwa nchini na kampuni ya Must International.

Alisema kampuni hiyo iliingiza kontena tano za unga wa ngano mwezi wa Novemba, mwaka jana, lakini moja lilipasuka njiani na kusababisha kuingia maji ya mvua yaliyoharibu unga huo.

Dk. Khamis alisema kipindi cha nyuma wafanyabiashara wengi walikukwa wagumu kulipia gharama za kuteketeza bidhaa zao zinapoharibika, lakini ziara zilizofanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman, Bandari ya Malindi zimewasaidia ZFDA kutekeleza majukumu yake.

Alisema kawaida Wakala wa Chakula na Dawa wanapogundua bidhaa imeharibika au kupitwa na muda wa matumizi hutoa ushauri kwa wafanyabiashara kuirejesha sehemu walikonunua ama kulipa gharama zote za kuiharibu hapa nchini na mara nyingi hukubali kulipa gharama za kuiharibu ili kupunguza gharama kubwa zaidi ya kuzirejesha zilikotoka.

Hata hivyo, katika kuwasaidia wafanyabiashara wa Zanzibar kuepuka kuingia gharama zisizo za lazima, Dk. Khamis aliwashauri kuwa waangalifu wanaponunua bidhaa kwa kuwa baadhi zinakuwa na muda mfupi kabla ya kumaliza muda wa matumizi.

Aliwataka kuhakikisha bidhaa wanazonunua wanazisafirisha kwa njia za uhakika na salama na zinaweza kufika nchini zikiwa na uwezo wa kutumiwa na wananchi kwa kipindi kisichopungua miezi sita bila kuharibika.

Aliwashauri baada ya kufika meli ya mzigo Zanzibar kufanya taratibu za kutoa mizigo yao bandarini ili kupunguza msongamano wa makontena na kuongezeka gharama za ushuru kwa kuendelea kukaa mizigo yao bandarini hapo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

## ANATAFUTWA DEREVA

Anatafutwa dereva wa kike mwenye uzoefu wa kuendesha Magari Mjini Dar es Salaam. Mwenye nia na kazi hiyo apige namba 0784691605/0715691605.

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA VYUMBA VIWILI INAJITEGEMEA, PLOT NA 712/1,BLOCK 46

MAWASILIANO 0787233272
0674927560

## TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSTITUTE

INATANGAZA MUHULA MPYA WA MASOMO KOZI,KILIMO,MIFUGO NA MAENDELEO YA JAMII.CHUO KIMESAJILIWA NA NACTE REG.PWF/041/ KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI. 0752761280/0767574701 AU WWW.TRACDI.AC.TZ

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Anuani ya Simu:"ARDHI"
Simu: 2548570 au 2502805
Telex 2271
(Makao makuu)

Baraza la Ardhi na Nyumba,
S.L.P 5058,
TANGA.

Unapojibu tafadhali taja: 30/12/2020
Kumb Na. Appl. No.6/2020

**YAH: SHAURI NA 6 LA 2020**

SAID HAMADUN BAKARI ……………...................MDAI
DHIDI YA
MGENI ATHUMAN RIKO & NA WENZAKE WATANO
…..........................................................................WADAIWA

**KWA: RAHMA ABDALLAH, ESTHER MAGEMBE, RAMADHANI SAID HABIBU, AISHA MOHAMED MAUMBA- POPOTE WALIPO**

Mwombaji tajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga.
Unaarifiwa kufika. Tarehe 21/1/2021 saa tatu kamili (3:00) asubuhi. Unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo kutolewa.Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na Hukumu kutolewa dhidi yako.
AMRI: hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuri/ lakiri ya Baraza hili leo tarehe 30/12/2020.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**TANGA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**FORM II**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo
CHAMWINO MJINI
Usimamizi wa mirathi NO. 01/2021.
Ombi la ERICK EVANCE MWAIPUNGU kuteuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu MARRY MADUMA MWAIPUNGU

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnano tarehe 18/01/2021 kabla huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Tarehe 15/01/2020.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.... OF 2020**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ARBOGAST APOLINARY SHIRIMA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ADELINA JOSEPH KATUNU**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 04/02/2021.
Dated at Dodoma this 04th day of 01/ 2021.

Presented for filling this 13/01/2021.

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER**
**MNADA WA HADHARA**

**DORAH MUHOMBA** ...............MDAI
DHIDI YA
**ELIAS MUHOMBA**...............MDAIWA

TUTAFANYA MNADA TAREHE 23/01/2021 SAA NANE MCHANA.-MAENEO YA KISASA WEST KWA IDHINI YA MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI SHAURI NO. 20/2017.TUTAUZA NYUMBA PLOT 75 BLOCK "J" ILI KUGAWA TALAKA.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER**
**MNADA WA HADHARA**

**EMMANUEL KOMBA**…. ...........MDAI
DHIDI YA
**ONE PLANET SCHOOL**….MDAIWA

TUTAFANYA MNADA TAREHE **16/02/2021** SAA NNE ASUBUHI.NYERERE SQUARE KWA IDHINI YA MAHAKAMA KUU KITENGO CHA KAZI SHAURI NO 02/2020.TUTAUZA GARI AINA YA COASTER 837 DPQ ILI KUFIDIA DENI ANALODAIWA NA EMMANUEL YOHANA.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER**
**MNADA WA HADHARA**

**CHIMA MAZENGO**…. ...............MDAI
DHIDI YA
**FELEX RICHARD**............….MDAIWA

TUTAFANYA MNADA TAREHE 23/01/2021 SAA NNE ASUBUHI.-MAENEO YA SWASWA MNARANI KWA IDHINI YA MAHAKAMA YA MWANZO MAKOLE SHAURI NO. 121/2019.TUTAUZA KIWANJA PLOT 13 BLOCK "F" ILI KUFIDIA DENI ANALODAIWA NA CHIMA MAZENGO.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER**
**TANGAZO LAMNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 16/02/2021 SAA NNE MCHANA WA KUUZA GARI AINA YA LAND CRUISER T 365 DMA MALI YA ANGELINA JOHN KINGWA, MAENEO YA NYERERE SQUAR BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.
**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## MATOKEO YA UCHAGUZI UGANDA 2021:

# Museveni Rais mteule Uganda na rekodi

**Kampala,** UGANDA

YOWERI Museveni ametangazwa kuwa rais mteule Uganda baada ya kupata ushindi wa kura asilimia 58.64.

Tume ya Uchaguzi Uganda (EC), imemtangaza Museveni kuwa mshindi wa uchaguzi mkuu uliofanyika Januari 14, mwaka huu. Kwa mujibu wa EC, Museveni alipata kura 5,851,037 sawa na asilimia 58.64 ya kura zote zilizopigwa.

Mpinzani mkuu wa Museveni, mwanamuziki Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, alishika nafasi ya pili kwa kupata kura 3,475,398 sawa na asilimia 34.83 ya kura zote.

Hata hivyo, Bobi Wine alitangaza kutokukubaliana na matokeo hapo jana wakati tume ya EC ilipokuwa ikiendelea kutangaza matokeo.Museveni awaonya wafuasi wa upinzani kutozua ghasia.

Museveni alionya kuwa vikosi vya usalama vitatumia nguvu kuzima juhudi zozote za ghasia baada ya kuchaguliwa kwake tena.

Museveni aliwaambia wanahabari katika kituo cha kitaifa cha kuhesabu kura nje ya mji mkuu Kampala kwamba hakuna atakayezua ghasia katika eneo hilo kwa sababu yeyote atakayejaribu kufanya hivyo atakabiliwa vilivyo.

**Mpinzani mkuu wa Museveni, mwanamuziki Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, alishika nafasi ya pili kwa kupata kura 3,475,398 sawa na asilimia 34.83 ya kura zote.**

Rais Museveni aliongeza kuwa hakuna mtu anayewashinda katika matumizi ya bunduki na pia mapigano.

David Rubongoya, Katibu Mkuu wa chama cha upinzani, National Unity Platform (NUP) kinachoongozwa na Bobi Wine ambaye jina lake rasmi ni Robert Kyagulanyi (pichani), aliyeshindwa na Museveni katika uchaguzi huo wa rais, aliliambia shirika la habari la DPA kwamba maofisa wa usalama wameanza kuwakamata wanachama na wafuasi wa chama hicho.

Katika taarifa, jeshi la polisi nchini Uganda limesema kuwa limewakamata takriban watu 84 kuhusiana na ghasia za uchaguzi.

Kupitia televisheni ya taifa, msemaji wa chama cha NUP, Joel Ssenyonyi alisema kuwa maofisa wa usalama walikuwa wakiwatesa washirika wa upinzani.

Ssenyonyi alisema kuwa Uganda iko kama katika vita, huku maofisa wa polisi na jeshi wakipelekwa kila mahali kuwakamata wafuasi wa upinzani.

Makazi ya Wine, msanii aliyegeuka kuwa mwanasiasa yaliyoko kwenye mji mkuu, Kampala yamezingirwa na wanajeshi tangu Ijumaa jioni na kumfanya kuwa chini ya kifungo cha nyumbani.

Wakati huo huo, Uingereza imetoa wito wa kuchunguzwa kwa malalamiko ya uchaguzi huo wa urais uliokamilika nchini Uganda baada Rais Museveni kutangazwa kuwa mshindi.

Waziri wa Uingereza anayehusika na masuala ya Afrika, James Duddridge, alisema kuwa raia wengi nchini Uganda na nje wameelezea wasiwasi kuhusu mazingira jumla ya uchaguzi huo kabla ya uchaguzi pamoja na mchakato mzima wa uchaguzi.



Duddridge alisema kuwa ni muhimu wasiwasi huo, kuchunguzwa na kutatuliwa kwa njia ya amani, kisheria na kikatiba.

Marekani kwa upande wake alisema wasiwasi ni kuhusu taarifa za ghasia na dosari zilizojitokeza katika uchaguzi huo mkuu wa Uganda.

Idadi kamili ya watu waliopiga kura ni 9,978,093 ikiwa ni sawa na asilimia 57.22 tu ya idadi ya watu waliojiandikisha kwenye daftari la wapiga kura.

Hii inamaana kuwa zaidi ya asilimia 40 ya waliojiandikisha hawakujitokeza kupiga kura.

Museveni, aliingia madarakani baada ya kutoka katika mapigano ya msituni mwaka 1986, na anatambulika kuwa kiongozi amedumu kwa muda mrefu zaidi barani Afrika.

Rais huyo mwenye miaka 76, aliweza kulifanya taifa hilo kuwa na amani kwa muda mrefu na kuleta maendeleo ambayo wengi wanafurahia.

Pia aliimarisha utawala wake kwa kuhamasisha utu na ushirikiano kutoa ajira , kuruhusu kuanzishwa kwa taasisi huru. Museveni ambaye anakuwa rais katika muhula wa sita, anaelekea kukaa madarakani kwa muda wa miaka 40, akiwa ni miongoni mwa marais waliokaa muda mrefu kuliko rais mwingine yeyote katika taifa hilo na katika eneo zima la Afrika Mashariki. **BBC/DW**

## Idadi waliopoteza maisha tetemeko la ardhi yafika 46

**Sulawesi,** INDONESIA

IDADI ya watu waliofariki kwenye tetemeko la ardhi lililotokea jana eneo la Majene, katika Jimbo la Sulawesi Magharibi mwa Indonesia imeongezeka hadi 46.

Mkuu wa Idara ya Mawasiliano ya Kituo cha Wakala wa Kitaifa wa Kudhibiti Maafa, Raditya Jati (pichani), alisema kuwa idadi kufikia sasa, ni 46 waliopoteza maisha kwenye tetemeko la ardhi huku 37 kati yao ni wa eneo la Mamuju na tisa ni wa eneo la Majene.



Raditya Jati pia aliongeza kusema kwenye taarifa yake kwamba idadi ya majeruhi imefikia 826.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopokewa hivi karibuni, jumla ya majengo 415 yanayojumuisha taasisi za umma kama hospitali, ofisi za magavana na usimamizi wa bandari, yalikumbwa na uharibifu.

Juhudi za utafutaji na uokoaji bado zinaendelea.

Shirika la Masuala ya Hali ya Hewa (BMKG) lilitangaza jana kuwa tetemeko la ardhi lenye ukubwa wa kipimo cha richta 6.2, lilitokea na kupiga kwa kina cha kilomita 10 na kilomita 6 Kaskazini Mashariki mwa mji wa Majene na miji ya Palu na Makasar. **TRT**



Viongozi wapya wa Marekani Joseph Biden na Makamu wake Kamala Harris, wanatarajiwa kuanza kazi rasmi baada ya kula kiapo wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

# Biden kutekeleza haya baada ya kuapa

**Washington,** MAREKANI

RAIS Mteule wa Marekani, Joe Biden, atasaini maagizo kadhaa ya kiutendaji siku ya kwanza baada ya kuapishwa kuiongoza nchi hiyo.

Biden anayetarajiwa kuapishwa Januari 20, mwaka huu, atakuwa rais 46 kuiongoza nchi hiyo.

Msaidizi wa ngazi ya juu wa Biden, Ron Klain, alisema kwamba maagizo ya kiutendaji yatahusu janga la virusi vya corona, uchumi wa Marekani unaodorora, mabadiliko ya tabia nchi pamoja na ubaguzi wa rangi.

"Majanga yote haya yanahitaji kushughulikiwa haraka," alisema Klain ambaye ni mkuu wa watumishi ajaye wa Biden.

Kwa mujibu wa Klain, katika siku zake 10 za kwanza madarakani, Biden atachukua hatua madhubuti kushughulikia mizozo hiyo minne, kuzuia madhara mengine ya haraka na yasiyoweza kurekebishwa pamoja na kuirudisha nafasi ya Marekani duniani.

Marekani ina takriban watu 400,000 waliokufa kutokana na ugonjwa wa COVID-19 na nchi hiyo inarekodi zaidi ya visa vipya milioni moja kwa wiki, wakati virusi hivyo vinazidi kuenea.

Wiki hii Biden aliuzindua mpango wa uokozi wa dola trilioni 1.9 kwa ajili ya kupambana na janga la virusi vya corona na kuufufua uchumi.

Kuchumi alisema siku ya kuapishwa Biden, kama alivyoahidi atasaini maagizo ya rais ni pamoja Marekani kujiunga tena kwenye Mkataba wa Paris wa Mabadiliko ya Tabia Nchi na kuibadili marufuku ya kuwazuia watu kutoka kwenye nchi kadhaa zenye waumini wengi wa Kiislamu kuingia Marekani, ambayo iliwekwa na Rais Donald Trump. **DW**

# POGBA KUTUA JUVE JULAI




**TURIN,** Italia

MABINGWA wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus itajaribu kutuma bei yao ya kumnunua Paul Pogba kutoka Manchester United mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa gazeti la Calciomercato.

Pogba anaonekana kujiandaa kuondoka United mwishoni mwa msimu huu wa 2020-21 baada ya wakala wake, Mino Raiola kudai kuwa kiungo huyo wa Ufaransa hana furaha pale Manchester.

Majaliwa ya Pogba yamekuwa mjadala mkubwa pale kwenye dimba la Old Trafford na ni wazi kwamba anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Pogba ameonyesha nia ya kutaka kurudi tena Turin ambako awali alicheza pale kabla ya kwenda Man United kwa mara ya pili.

Real Madrid na Paris Saint-Germain zimekuwa zikihusishwa na mchezaji huyo, lakini Juve, ambayo ilimsajili Pogba kutoka United mwaka 2012 kabla ya kumpoteza tena kwa 'Mashetani Wekundu' hao miaka minne baadaye, wanataka kumleta tena mshindi huyo wa Kombe la Dunia pale Turin.

# Lampard bado ana imani na Werner

**LONDON,** England

FRANK Lampard bado ana imani na Timo Werner licha ya straika huyo kuendelea kuwa na ukame wa mabao kwenye Ligi Kuu England, hasa baada ya kukosa nafasi ya kufunga wakati Chelsea ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Fulham.

Ingawa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani alifunga bao kwenye mchezo wa hivi karibuni wa Kombe la FA dhidi ya Morecambe, alikwenda kwenye mchezo huo wa juzi Jumamosi bila ya bao katika mechi tisa za ligi sasa.

Tayari ulikuwa muda mrefu sana wa kucheza bila kufunga bao, tangu alipocheza mechi 11 bila kufunga mwaka 2016.

Alikuwa na nafasi nzuri ya kufunga kwenye mchezo huo, lakini alikosa nafasi hiyo wakati akiwa yeye na golikipa wa Fulham, Alphonse Areola.

Bahati nzuri ni kwamba, Chelsea na Lampard, tayari walikuwa wameshapata bao kupitia kwa Mason Mount.

Wakati alipoulizwa kama ana hofu kuhusu Werner, Lampard aliiambia Sky Sports: "Nafikiri ni kitu cha kawaida.

"Kama hufungi mara kwa mara kama anavyotaka, alifunga wiki iliyopita kwenye FA. Amekuwa akijituma sana, lakini naamini bado ana nafasi ya kufanya vizuri."




# *Ozil: Situndiki daluga nikiondoka Arsenal*



**LONDON,** England

MESUT Ozil amesema hana nia ya kustaafu atakapoondoka Arsenal, na mapenzi yake ni kuhamia Fenerbahce au soka la Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani yuko kwenye siku za mwisho za pale kunako klabu ya Arsenal.

Ozil hajaichezea Arsenal tangu Machi, licha ya kuonekana yuko fiti, na limebaki kuwa swali kama ataondoka Januari hii au mwishoni mwa msimu.

Mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid alijihusisha kwenye mitandao ya kijamii na alifanya kikao cha maswali na majibu kwenye Twitter, Jumatatu.

Alijibu maswali kwenye mada zilizokuwa zikijadiliwa, na moja ikiwa kwamba hakujuta kujiunga na Arsenal.

Ozil pia aliulizwa ikiwa ana mpango wa kustaafu atakapoondoka Arsenal, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, hakuwa na shaka katika majibu yake.

"Sitafanya hivyo," alisema alipoulizwa ikiwa angecheza baada ya kuondoka Arsenal. "Kuna nchi mbili ambazo ninataka kucheza mpira kabla ya kustaafu: Uturuki na Marekani."

# Rivaldo awachambua Koeman, Zidane LaLiga

**SAO PAUL,** Brazil

RIVALDO amesema Ronald Koeman anastahili zaidi pongezi tangu alipochukua kibarua cha kuinoa Barcelona, kuliko Zinedine Zidane akiwa Real Madrid.

Kwa mujibu wa Rivaldo, Koeman amefanya kazi nzuri sana na ngumu ya kuwaunganisha vijana kikosini tofauti na Zidane.

Lakini anamuona kama Zidane anafanya kinyume kabisa na mwezake, kwa kutowapa zaidi kipaumbele vijana na kuhakikisha bado wanaendelea kuwa na ushindani.

Kwa mtazamo wake Zidane anawapa shinikizo kubwa wachezaji, kitu ambacho si kizuri katika kuwaongoza wachezaji vijana.

"Wakati wote nimekuwa nikisema kuwa namna pekee ya kuongoza vipaji chipukizi ni kutowawekea shinikizo kubwa dhidi yao, na nadhani kwa suala hili Koeman anafanya vema zaidi," alisema Rivaldo akinukuliwa na ESPN.

"Koeman ameweza kuwaunganisha vijana pamoja na kina Busquets, Messi, Jordi Alba. Koeman anastahili kupongezwa na kuheshimiwa kwa hilo.

"Sifahamu nini kipo nyuma ya hili, lakini Zidane anafanya kinyume chake kwa alivyofanya kutowatumia vema vipaji chipukizi kama Valverde, Rodrygo au Vinicius."

Rivaldo anamtazama Zidane kama uongozi wake unakuwa katika namna ya kuwakomoa wachezaji na kwa wakati mwingine hilo linakuja kuathiri timu na siyo mchezaji pekee.






# MARTINEZ KUJIFUNGA INTER

**MILAN,** Italia

LAUTARO Martinez yupo kwenye hatua nzuri ya kufikia makubaliano mapya ya kuongeza mkataba na Inter Milan na kuzima uvumi juu ya mpango wake wa kutaka kuondoka.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2023, lakini Inter inataka kumfunga kwa mkataba mpya.

"Nina furaha InterMilan ni jiji kubwa," aliiambia Sportweek. "Wakala wangu na klabu wanazungumza na nina utulivu.

"Ninataka tu kutoa kila kitu kwa Inter, kisha tutafikia makubaliano."

Lautaro alikuwa akihusishwa na kuondoka kwa Inter, lakini anajaribu kuweka sawa uvumi juu ya uhamisho wake.

Lautaro anacheza pamoja na Lionel Messi kwenye timu ya Taifa ya Argentina na alikuwa akihusishwa na mpango wa kuungana naye kule Barcelona.

"Ilikuwa ndoto kubwa kwangu," Lautaro alisema. "Inashangaza kucheza naye, ndiye mchezaji bora zaidi duniani na nina bahati ya kucheza naye kwenye timu ya taifa. Yeye ni msukumo kwa wachezaji wachanga."

# *Dembele atamani kuwa kama Torres*

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI mpya wa Atletico Madrid, Moussa Dembele, amesema kuwa Fernando Torres alikuwa ni alama yake tangu alipokuwa mtoto.

Dembele ametua hapo kuchukuwa nafasi ya Diego Costa ambaye amesitisha mkataba wake mwezi uliopita, na mshambuliaji huyu mpya anatarajiwa kuwa sehemu muhimu ya Atletico.

Dembele amefunga jumla ya mabao 44 kwa misimu yake miwili alipokuwa na Lyon, ambao alijiunga nao mwaka 2018 akitokea Celtic.

Msimu huu haujawa mzuri sana kwake akiwa ameona nyavu mara moja tu kwa mechi zake 16 alizocheza kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Dembele ameelezea kuwa mpango wake yeye kwenye klabu yake mpya ni kufunga mabao, kwa kuwa hiyo ndiyo kazi yake, lakini amesisitiza kuwa gwiji wa Atletico, Torres ndiye aliyekuwa akimvutia zaidi tangu alipokuwa mtoto.

"Kimsingi, mimi ni straika na ninapenda kufunga mabao. Hiyo ndiyo kazi yangu. Napenda kutengeneza nafasi, kupokea mipira na kufunga.

"Ni mchezaji mzuri mwenye mbinu. Ninasubiri kwa hamu kuanza kucheza hapa, nilipokuwa mtoto Fernando Torres ndiye niliyempenda, alikuwa ni mfano wangu wa kuigwa, hivyo nina furaha kuwa hapa."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR NA MTIRIRIKO WA KULIKIMBIA SOKA

●●● Kilifika kipindi ninajiuliza mwenyewe kwa nini niendelee kucheza kama watu hawapendi...

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain na Brazil, Neymar, amebainisha alifikiria kustaafu kucheza soka.

**Neymar anatajwa kama mmoja wa wachezaji bora duniani, lakini staili ya maisha yake nje ya dimba imekuwa ikipamba zaidi vyombo vya habari na kuonekana haiendani na mchezo wenyewe.**

Mchezaji huyo ghali zaidi katika historia ya usajili baada ya kujiunga na PSG kutoka kwa miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barcelona kwa euro milioni 222 mwaka 2017, Neymar amekiri kuwa shutuma dhidi yake zilimuathiri.

"Kamwe sitapoteza mapenzi yangu na soka, lakini kuna wakati nilitaka kabisa kuachana na kucheza," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 akiliambia jarida la Gaffer Magazine.

"Ilifika kipindi ninajiuliza mimi mwenyewe kwa nini niendelee kucheza kama watu hawapendi.

"Nilikuwa narudi nyumbani kichwa kimewaka moto na nikakumbuka kila kitu nilichofanya kwenye soka.

"Napenda soka na ndio sababu hasa iliyonituliza na kuamua kubaki kuendelea kucheza.

"Kwa sababu nina bahati. Kiukweli kabisa. Nimefanikiwa kwa vitu vingi sana katika kipindi changu cha uchezaji ambapo imenifanya mimi na familia yangu kuwa na furaha ya aina yake.

"Hasa nilipoanza kuichezea Santos FC, na kushinda taji la kwanza na Santos, kushinda Kombe la Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini) ilikuwa muhimu sana kwangu.

"Kujiunga na Barcelona ilikuwa ni ndoto yangu tangu nilipokuwa mdogo, kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na ujio wangu hapa Paris. Nyakati zote hizo zitabaki kuwa kumbukumbu bora sana kwangu."

Neymar aliongeza: "Kamwe sikuhisi presha. Mimi ni mtu ambaye naweza kuituliza presha yangu; kuwa namba 10 kwa timu ya Taifa ya Brazil, namba 10 hapa PSG ni jambo la kujivunia mimi kama Neymar.

## ZISIKUPITE

### JUVE KUMSAJILI POGBA JULAI

JUVENTUS itatuma maombi ya kumsajili kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, 27, kipindi cha majira ya joto kijacho wakati ambao wanaamini klabu hiyo ya Old Trafford itapunguza bei ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, ambaye mkataba wake unamalizika majira ya joto 2022. ***(Calciomercato, via Sunday Express)***

### RICE HAKIJAELEWEKA CHELSEA

KOCHA wa West Ham, David Moyes, amesema Chelsea na Manchester United hazijawasilisha ombi la kutaka kumsajili kiungo, Declan Rice, 22, baada ya klabu hizo kuhusishwa na nyota huyo wa kimataifa wa England. ***(Amazon, via Mail on Sunday)***

### WIJNALDUM KUKATAA MKATABA

MKATABA wa kiungo wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum, 30, unamalizika kipindi cha majira ya joto kijacho, amekataa mkataba mpya ili kutimiza ndoto yake ya kujiunga na Barcelona. ***(Sunday Mirror)***

### ASTON VILLA KWA MORGAN

ASTON Villa imefungua mazungumzo na Marseille kwa ajili ya dili la Morgan Sanson mwenye umri wa miaka 26 raia wa Ufaransa. ***(Mail)***

### GRACIA HAONDOKI JANUARI

MLINZI wa Manchester City, Eric Garcia, 20, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto, amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda Barcelona, lakini uhamisho kwa nyota huyo hautaweza kufanyika Januari hii, baada ya uchaguzi wa urais kule Nou Camp kuahirishwa hadi Machi. ***(Manchester Evening News)***

### WILSHERE KUPEWA MKATABA

KLABU ya Bournemouth inaweza kuwa tayati kutoa ofa kwa kiungo wa zamani wa Arsenal na England, Jack Wilshere,29, ambaye anafanya mazoezi na klabu hiyo baada ya kuondoka West Ham. ***(Talksport)***

### MALEN AWANIWA DORTMUND

BORUSSIA Dortmund inamfuatilia straika wa PSV Eindhoven mwenye umri wa miaka 21, Donyell Malen, ambaye anawaniwa na Arsenal, kama mrithi wa winga, Jadon Sancho endapo nyota huyo wa timu ya Taifa ya England ataondoka. ***(Soccer News, via Daily Star on Sunday)***

### DHANDA AGOMBEWA ENGLAND

LEEDS United na Bournemouth zinawania kumsajili kungo wa Swansea City, Yan Dhanda, 22. ***(Mail)***

### CAMARA AWINDWA EPL

KLABU kadhaa za Ligi Kuu England, zinamuwania kiungo wa Benfica, Ronaldo Camara,18, baada ya nyota huyo kutokuwa na namba Benfica. ***(Mail)***

### INGS, BERTRAND NA MIKATABA

KOCHA wa Southampton, Ralph Hasenhuttl amesema klabu hiyo haitacheza "kamari" kwenye mishahara ya wachezaji wakati huu wakiwa kwenye mazungumzo ya kuongeza mkataba na nyota wao wawili, Danny Ings, 28, na Ryan Bertrand, 31. ***(Mail on Sunday)***

# Matola amtabiria makubwa Lwanga

**Na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola, amemwagia sifa kiungo mkabaji mpya wa timu hiyo, Taddeo Lwanga kuwa ni mzuri dimbani na muda si mrefu atatajwa kuwa mmoja kati ya viungo bora na hatari kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Matola (pichani), ambaye wakati akicheza soka kwenye klabu ya Simba alikuwa akicheza kama kiungo mkabaji, namba ambayo anaicheza Lwanga, alisema hakutegemea kama Lwanga angecheza kwa kiwango kikubwa vile wakati akiwa hajacheza soka la ushindani kwa muda mrefu.

Alisema ni muda tu unahitajika, lakini baadaye atakuwa msaada mkubwa kwa klabu ya Simba kwenye michuano mbalimbali ambayo itacheza.

"Nafikiri atakuwa kiungo bora na hatari kwenye ligi yetu. Ni mtu ambaye kiukweli ana uwezo mzuri. Ana umbile zuri, mpambanaji na mtu ambaye anaujua sana mpira," alisema Matola.

Alisema kwenye mechi ya kwanza hakufanya vema kwa sababu alikuwa hajafanya mazoezi kwa muda mrefu kutokana na kuugua.



"Tulimchukua akiwa hajafanya mazoezi, alikuwa anaugua na hata huko alikotoka kwa muda mrefu alikuwa hajacheza soka la ushindani, tulienda naye Kombe la Mapinduzi akiwa hajafanya mazoezi mwezi mzima. Mechi ya kwanza hakufanya vizuri, lakini mechi ya pili na Namungo alicheza vema, na mechi ya fainali dhidi ya Yanga kila mtu sasa atakuwa shuhuda wa kile ambacho alikifanya," alisema Matola.

Simba ilimsajili mchezaji huyo kama mbadala ya Mbrazil Gerson Fraga ambaye kwa sasa ni majeruhi na yupo kwao, Brazil akiendelea na matibabu.

Lwanga ambaye alikuwa akiichezea klabu ya Tanta FC ya nchini Misri, pia ni mchezaji wa timu ya Taifa ya Uganda, Uganda Cranes.

# ZAHERA APEWA MIKOBA YA FLUGENCE GWAMBIANA FC



**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Gwambina FC, umesema timu hiyo itaingia kambini wiki hii huku ikinolewa na Mkurugezi wa Ufundi, Mwinyi Zahera, ambaye ataendelea na majukumu ya kukinoa kikosi hicho kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Gwambina FC, Daniel Kilai, alisema timu hiyo itaanza mazoezi huku mchakato wa kutafuta kocha mkuu ukiendelea.**

Alisema mpango wao ni kuhakikisha mchakato huo wa kutafuta kocha mkuu unamalizika ndani ya wiki hii kwa kuingia makubaliano na kuanza kazi mara moja.

"Kikosi kitaingia kambini Januari 20, (Jumatano), ikiwamo wachezaji tuliowasajili dirisha dogo ambao ni Mrisho Ngassa, Salim Aiyee na Mohammed Mussa kutoka Zanzibar.

"Mazoezi yataendelea na kusimamiwa na Mwinyi Zahera, huku tukipambana na mchakato huo kupata kocha mkuu ndani ya wiki hii," alisema Kilai.

Alisema malengo yao ni kupata kocha mkuu ambaye ataendana na vigezo vyao ikiwamo kuhakikisha wanaendelea kubaki katika mikikimikiki ya Ligi Kuu kwa kumaliza katika nafasi ya tano.

Uongozi wa Gwambina FC ulimtimua Kocha Mkuu, Flugence Novatus, mwanzoni mwa mwezi huu baada ya kutoridhishwa na matokeo ya timu hiyo kwa ujumla.

## WAMEANGUKIA HUKU...



Mshambuliaji wa zamani wa Simba na Yanga, Amissi Tambwe (kulia), akiwa amepozi katika picha na kiungo wa zamani wa Arsenal ya England, Barcelona ya Hispania na Cameroon, Alex Song, walipokutana nchini Djibouti ambako wote wanacheza kwa sasa Ligi Kuu ya huko. Tambwe (32), anaichezea ASC Police Nationale, wakati Song (33), yeye anaichezea Klabu ya Arta/Solar7. **PICHA: MTANDAO**

# *Nyota wa majaribio Simba watemwa*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umeamua kuachana na mpango wa kuwasajili nyota watatu waliokuwa wakifanya majaribio na timu hiyo kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi iliyomalizika Jumatano iliyopita.

Nyota hao ni Bernard Agele, Kelvin Moyo na Ian Nyoni ambao walikuwa miongoni mwa wachezaji walioifikisha Simba katika fainali ya michuano hiyo iliyofanyika visiwani Zanzibar.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili kutoka chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, zimeeleza kuwa tayari nyota hao wameondoka jana asubuhi kurejea makwao.

"Agele kaondoka leo asubuhi (jana) na wengine wawili Moyo na Nyoni waliondoka usiku, aliyebaki ni mshambuliaji wa FC Platinum ya Zimbabwe, Perfect Chikwende, ambaye tayari usajili wake umefanyika na kutangazwa.

"Wale waliocheza Kombe la Mapinduzi wameondoka kutokana na kutolivutia benchi la ufundi, Chikwende anasubiri Ijumaa hii kujiunga na wachezaji wenzake kwa ajili ya mazoezi ya kujiandaa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika," kilieleza chanzo chetu.

Alipoulizwa Kocha Msaidizi, Selemani Matola, alisema nyota hao walikuwa katika majaribio, hivyo lolote linaweza kutokea na uongozi utafuata mapendekezo ya benchi la ufundi kulingana mahitaji ya timu katika usajili.

"Walikuwa katika majaribio na viongozi wamesajili kulingana na mahitaji ya timu, tumemaliza Mapinduzi na tumerejea na tumewapa mapumziko ya wiki moja na Ijumaa hii tunaingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya Ligi Kuu na michuano ya kimataifa," alisema Matola.

# Michezo



Jumatatu Januari 18, 2021

Nipashe


Neymar na mtiririko wa kulikimbia soka UKURASA 22

# CHIKWENDE KATIKATI YA MORRISON, KAHATA

## ●●● Aapa kupigania namba huku akiwataja Miquissone, Bwalya na Kapombe, lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI akifurahia kuwa miongoni mwa nyota watakaounda kikosi cha mabingwa wa Ligi Kuu Bara na kuahidi kupambana na ushindani uliopo, winga mpya wa Simba, Mzimbabwe Perfect Chikwende, ameendelea kuwa katikati ya nyota wawili wa timu hiyo, Bernard Morrison na Francis Kahata.

**Simba inatarajiwa kutangaza kukata mchezaji mmoja kati ya 10 wa kimataifa ili kumwezesha Chikwende kucheza Ligi Kuu na kama itashindwa kufanya hivyo, nyota huyo aliyejiunga na 'Wekundu wa Msimbazi' hao akitokea FC Platinum ya Zimbabwe, ataichezea kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa pekee.**

Nyota wa kimataifa wa Simba ambao wapo kwenye usajili wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa ni Pascal Wawa (Ivory Coast), Joash Onyango na Francis Kahata (Kenya), Bernard Morrison (Ghana), Rally Bwalya na Clatous Chama (Zambia), Chris Mugalu (DR Congo), Meddie Kagere (Rwanda), Luis Miquissone (Msumbiji) na Taddeo Lwanga (Uganda).

Simba inatakiwa kuengua mchezaji mmoja kwenye orodha ya watakaocheza Ligi Kuu kutokana na kanuni ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuruhusu kila klabu kuwa na wachezaji 10 tu wa kigeni waliosajiliwa kushiriki ligi hiyo.

Hata hivyo, licha ya uongozi wa Simba kutoweka wazi hadi sasa kuhusu mchezaji itakayemuengua ili kumpisha Chikwende kuitumikia klabu hiyo kwenye Ligi Kuu Bara, Morrison na Kahata, wamekuwa wakihusishwa zaidi mmoja kumpisha winga huyo wa Zimbabwe.

Taarifa kutoka chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, zimeeleza: "Anaweza kuwa Morrison ama Kahata, lakini bado uamuzi rasmi haujafikiwa, tunataka kufanya hivyo ili kumwezesha Chikwende kuzoeana vizuri na wenzake uwanjani."

Lakini kwa upande wa Chikwende akizungumzia usajili wake, alisema ni mwenye furaha kujiunga na Simba na ni moja ya timu nzuri yenye ushindani mkubwa, hivyo atajitahidi kupambana ili kupata nafasi.

"Kwa ujumla ni mwenye furaha, timu ni nzuri, kuna ushindani mkubwa ambao utaboresha wasifu wangu, nitapambana ili kupata kiwango changu bora," alisema mchezaji huyo ambaye aliifunga Simba wakati FC Platinum ikishinda bao 1-0 nyumbani kwenye mechi ya kwanza ya raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika kabla ya Wekundu wa Msimbazi hao kupindua matokeo Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kushinda 4-0 mechi ya marudiano.

Kuhusu majina ya wachezaji anaowafahamu ndani ya timu yake hiyo mpya, Chikwende aliwataja Luis Miquissone, Clatous Chama, Rally Bwalya na Shomari Kapombe, ikionyesha bado ana kumbukumbu ya namna nyota hao walivyowasumbua wakati walipokutana kwenye mechi ya marudiano jijini Dar es Salaam Januari 6, mwaka huu.

"Luis, Chama, Bwalya na Kapombe ni baadhi ya wachezaji ninaowafahamu katika klabu ya Simba," alisema Chikwende hadi sasa ana mabao mawili kwa jina lake kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Katika mechi hiyo ya marudiano, mabao yalifungwa na Erasto Nyoni (penalti), Kapombe, John Bocco na Chama (penalti) huku Miquissone na Bwalya wakionyesha kiwango cha juu.

Matokeo hayo yameipeleka Simba hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa ambapo sasa imepangwa Kundi A pamoja na Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan.



Wachezaji wa Taifa Stars wakiwa mazoezini nchini Cameroon kujiandaa na michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambapo kesho watashuka katika Uwanja wa Limbe/Buea nchini humo saa moja usiku kuvaana na Zambia. **MPIGAPICHA WETU**

# Nyoni aiwahi Zambia CHAN

**Na Mwandishi Wetu**

BEKI wa kati wa Simba na timu ya Taifa, Taifa Stars, Erasto Nyoni, amewasili salama nchini Cameroon na kujiunga na kikosi cha timu hiyo ambacho kesho kitashuka dimbani dhidi ya Zambia kwenye mechi yao ya kwanza ya Kundi D ya michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Nyoni hakusafiri pamoja na wachezaji wenzake kutokana na kukabiliwa na matatizo ya kifamilia, lakini jana mchana aliwasili Cameroon na kujiunga na kikosi hicho tayari kwa mechi hiyo itakayopigwa kesho kwenye Uwanja wa Limbe/Buea majira saa moja usiku.

Akizungumza na Nipashe kutoka Cameroon jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Clifford Ndimbo, alisema tayari Nyoni amewasili Cameroon na kujiunga katika kambi ya Stars.

"Amewasili leo mchana (jana) na moja kwa moja amejiunga na wenzake tayari kwa maandalizi ya michuano inayotukabili, ambapo keshokutwa (kesho) tutacheza dhidi ya Zambia," alisema.

Kuhusu maandalizi ya timu hiyo, Ndimbo alisema yanaendelea vizuri na morali ya wachezaji iko juu kwa timu nzima.

"Kwa ujumla morali ipo juu na kocha anaendelea na maandalizi na anaamini timu itafanya vizuri katika mashindano haya," Ndimbo alisema.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042